# TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA MBILI ZA KISWAHILI

NA

BEATRICE MWENDERANI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI IDARA YA ISIMU NA LUGHA

University of NAIROBI Library

0389612 3

JULAI, 2012

## IKIRARI

Tasnifu ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile,kwa minajili ya kutosheleza shahada ya uzamili.

**MTAHINIWA**

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 23/10/2012

**BEATRICE MWENDERANI**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu sisi tulioteuliwa na chuo kikuu kusimamia

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 25-10-2012

**DKT. MWANGANGI WA MUSYOKA**

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 23-10-2012

**DKT. EVANS MBUTHIA**

# TABARUKU

Tasnifu hii nimewatabarukia wanangu wapendwa Sharon Muhonja na Esteen Andanyi.

Mungu awalinde, awatunze na awaneemeshe.

## SHUKRANI

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Maulana kwa kunijalia kuishi,kufikia umri huu na kusoma hadi kiwango hiki cha uzamili. Kama siye Mwenyezi Mungu hakuna lolote zuri ambalo ningefanya. Amenihifadhi, akanilinda na kunionyesha njia ya kufaulu maishani. Shukrani zangu pia ziwaendee wazazi wangu wapendwa baba Jamen Okudo Keronze na mama Ruth Alividza Okudo kwa kunizaa, kunilea, kunishauri na kunielimisha. Wapendwa hawa ndio walionifungulia mlango wa kusoma na kunionyesha uzuri wa masomo. Nashukuru kwa maombi yao kila wakati. Nazidi kuwashukuru sana kwa mchango wao katika kuwakuza wanangu wakati nilipokuwa masomoni nikisomea digrii yangu ya kwanza. Sitasahau kuwashukuru wanangu wapendwa Sharon Muhonja na Esteen Andanyi kwa kunipa fursa ya kusoma. Mlinihimiza na kunipa moyo wa kuona siku nyingine mpya nilipokuwa karibu kukata tamaa. Mungu awaneemeshe na awape ari ya kusoma mfikie viwango vya juu katika masomo.

Sitakosa kuwashukuru ndugu zangu na dada zangu kwa msaada wao wote walionipa wa kifedha na hata kwa mawaidha. Nao ni Benard, Gilbert, George, Geoffrey, Sammy, Canaam, Pamela na Josline. Shukrani zangu ziwaendee ndugu Benard na Gilbert kwa kuhakikisha kuwa masomo yangu yalikamilika bila tashwishi. Namshukuru pia ndugu yangu mdogo Geoffrey kwa jukumu lake la kuwatunza wanangu kwa muda huo wote. Namwombea baraka za Mungu na ufanisi maishani.

Shukrani zangu ziendee tume ya kuwaajiri walimu T.S.C. kwa kunipa likizo ili nikamilishe ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili. Sitawasahau walimu wote

niliofunza nao katika shule ya mseto ya Kibuye, Kisumu. Endeleeni na moyo uo huo na Mungu awabariki. Namshukuru sana mwalimu Suleman wa chuo cha Ualimu cha Eregi kwa msaada alionipa Mungu akubariki. Nawapongeza sana wasimamizi wangu katika idara ya isimu na lugha kwa ushauri wao na kuboresha kazi yangu. Pongezi Dkt. Mwangangi wa Musyoka na Dkt. Evans Mbuthia kwa ushauri na juhudi zenu za kuhakikisha kazi yangu imekuwa bora zaidi. Nawashukuru pia wahadhiri walionielekeza darasani na kunifunza kukifahamu Kiswahili zaidi. Nao ni Prof. John Habwe, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Abdulaziz, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt.. Zaja Omboga, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Tom Olali, na Bwana Mungania.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiri nao jahazi hili la ufanisi katika Chuo Kikuu Cha Nairobi. Safari ilikuwa ndefu lakini tulitiana moyo na kusaidiana kama wana wa mzazi mmoja. Mtakuwa ukumbusho mwema katika maisha yangu. Neema za Mwenyezi Mungu ziandamane nanyi daima. Nao ni Pauline Wangechi Kimani, Zipporah Nyaboke Rori, Everlyne Were, Jackline Muthuri, Ferinda Kiende, Shadrack Amolloh na Joseph Kiongera.

Mwisho ningependa kuwashukuru wafuatao kwa kuhakikisha kuwa kazi yangu ilichapishwa na kukamilika kwa wakati Njeri wa Chuo Kikuu cha Nairobi, Linda, na Sheique Oloo wote wa Kisumu. Mungu awabariki kwa kazi yenu nzuri.

# IKISIRI


Utafiti huu umeshughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia mbili za Kiswahili. Tumeangalia picha ambayo mwanamke amepewa na jamii katika tamthilia za *Kilio Cha Haki (*1981*)* na *Pango(*2003*)*.

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia tatizo la utafiti,madhumuni ya utafit,nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa juu ya mada na njia za utafiti.

Katika sura ya pili tumeshughulikia taswira hasi na chanya aliyopewa mwanamke na jamii katika tamthilia ya *Kilio cha Haki (1981)* Alamin Mazrui na kisha tukaangazia njia ambazo mwanamke anaweza kuzitumia ili kujikomboa.

Sura ya tatu imeshughulikia taswira chanya na hasi aliyopewa mwanamke na jamii katika tamthilia ya *Pango* (2003) Wamitila K.W na vilevile tukaonyesha njia ambazo mwanamke anaweza kutumia ili kujikomboa.

Sura ya nne imeshughulikia hitimisho la utafiti wetu pamoja na mapendekezo.

# YALIYOMO

Ukurasa

IKIRARI ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

IKISIRI ........ vi

YALIYOMO ........ vii

**SURA YA KWANZA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 3

1.4 Nadharia Tete ........ 4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 4

1.6 Upeo na Mipaka ........ 5

1.7 Msingi wa Nadharia ........ 6

1.7.1 Mirengo ya Ufeministi ........ 10

1.8 Yaliyoandikwa juu ya mada. ........ 11

1.9 Njia za utafiti ........ 17

**SURA YA PILI ........ 18**

2.0 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA *KILIO CHA HAKI (1981)* ........ 18

2.1 Utangulizi ........ 18

2.1.1 Mwanamke kama binadamu asiyezingatia maadili ........ 19

2.1.2 Mwanamke kama kiumbe asiye na mielekeo inayofaa ........ 23

2.1.3 Mwanamke kama kiumbe dhalili ........ 25

2.1.4 Mwanamke kama kiumbe aliyekandamizwa na utamaduni ........ 27

2.1.5 Mwanamke kama binadamu anayestahili kuadhibiwa ........ 31

2.2 Mwanamke kama kiumbe jasiri na mwenye msimamo thabiti ........ 39

2.2.1 Nafasi ya mwanamke katika jamii ........ 41

2.2.2 Mwanamke kama kiumbe mwenye mapenzi ya dhati ........ 43

2.2.3 Mwanamke kama mfanyikazi anayewajibika....4
2.2.4 Mwanamke kama mwanamapinduzi ....4
2.2.5 Mwanamke kama kiumbe aliye na uwezo wa kujitetea ....4
2.2.6 Kimalizio ....4

**SURA YA TATU....4**
3.0 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA YA PANGO ....4
3.1 Mwanamke kama mwanamapinduzi ....4
3.1.1 Mwanamke kama mtunzi wa jamii....5
3.1.2 Mwanamke kama kiumbe jasiri na mwenye msimamo thabiti ....5
3.1.3 Mwanamke kama kiongozi shupavu ....5
3.1.4 Mwanamke kama kiumbe msomi....5
3.1.5 Mwanamke kama mkombozi wa jamii....5
3.1.6 Mwanamke ni kiumbe aliye na uwezo wa kujitetea....5
3.1.7 Mwanamke kama kiumbe anayepinga mila zilizopitwa na wakati ....6
3.1.8 Mwanamke kama kiumbe aliye na uwezo wa kuwaunganisha wenzake ....6
3.1.9 Mwanamke kama Kiumbe anayewajibika....6
3.1.10 Mwanamke kama kiumbe aliyeelimika....6
3.1.1 Mwanamke kama mzalendo ....6
3.2 Mwanamke kama kiumbe asiye na haki ya kuwania uongozi....6
3.2.1 Mwanamke kama kiumbe dhalili....6
3.2.2 Mwanamke kama kiumbe kinachokandamizwa na utamaduni ....6
3.2.3 Vitisho vinavyomkabili mwanamke....7
3.2.4 Mwanamke kama kiumbe asiye na msimamo thabiti....7
3.2.5 Kimalizio ....7

**SURA YA NNE ....7**
4:0 HITIMISHO ....7
4.1 Mapendekezo....8

**MAREJELEO ....8**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Mada hii imetathmini taswira ya mwanamke katika *Kilio Cha Haki* (1981) kilichoandikwa na Alamin Mazrui na *Pango* (2003) kilichoandikwa na Wamitilia K. W. Katika kazi hizi tumegundua kwamba jamii nyingi zimeendelea kumdhulumu mwanamke na kumchukulia kama chombo cha kumtumbuiza mwanamume na kulea watoto. Mwanamke anachukuliwa kama kiumbe duni na asiyestahili kuheshimiwa na kupewa hadhi na kila mtu. Anadhulumiwa na kubezwa kwa sababu mwanamume amepembezwa na jamii na kupewa mamlaka mengi na hivyo sharti mwanamke awe chini yake.

Katika *Kilio Cha Haki (*1981*)* Lanina aliwaongoza wafanyakazi katika mgomo uliosababisha hasara kubwa katika shamba la bwana Delamon. Lanina anawahamasisha wenzake kuhusu haki zao na kuwahimiza kushiriki katika mgomo ili kumshinikiza`Delamon kuboresha hali ya kazi.Lanina anakumbana na matatizo mengi.Anazuiliwa kizuizini na kupigwa na askari ili awachane na mgomo lakini anaapa kutowasaliti wenzake.

Katika tamthilia ya *Pango (*2003) Katango anajitokeza kama mwanamke shupavu na kushiriki katika siasa ili kuleta mabadiliko katika Pango.Licha ya vitisho kutoka kwa Ngwese na wafuasi wake Katango alibaki imara na kupigania haki ya wana Pango.Mwishowe akaikomboa nchi yake.

Friedman. B. (1963) katika Gaskofu: *Roles Women Play*, anaeleza kuwa mwanamke anafaa aheshimiwe kwake nyumbani na hata nje ya nyumba yake na wanajamii. Anaendelea kusema kuwa katika jamii zetu wanawake wananyanyaswa kupitia kwa vyombo vya mawasiliano kama magazeti au katika runinga.Wanawake wanaonekana wakitangaza bidhaa mbalimbali wakiwa katika vikundi na hata wakiwashawishi watu kununua.

Engels (1950) katika *The Origin of the Family, Private Property* anaeleza kuwa kuna mtagusano baina ya umaksi na ufeministi. Anasema kwamba wanawake na wanaume walikuwa na usawa.Kila kundi lilikuwa na uhuru wao.Baadaye wanawake walipoteza uhuru wao wa asili na kulazimishwa katika nafasi ya kuwategemea wanaume.Kuanzia wakati huo mwanamume aliwakilisha nguvu za uchumi.

Wakati ng`ombe waliomilikiwa na mwanaume walianza kuleta mali, wanaume waliyamiliki mali hayo na wakawa ndio wenye mamlaka, kulingana na Engels kazi za wanaume za uwindaji na ufugaji zilianza kuleta faida kuliko kazi za nyumbani. Ongezeko la mali upande wa baba ulizusha kuwepo kwa mali ya kibinafsi na hivyo wanawake wakaanza kuwategemea wanaume kiuchumi.

Mali yaliyomilikiwa na wanaume hayangerithishwa watoto wa kiume iwapo baba wa mtoto huyo hakujulikana rasmi kiuzazi. Uchumi ulibadilisha mfumo wa familia kutoka kwa jamii nzima hadi kwa ushirikiano wa watu wawili na kwa mke na mume. Wanawake wakawa kama, ng'ombe, mali ya wanaume. Ni kutokana na maelezo ya Engels ndiposa

tunaazimia kutathmini iwapo maoni yake bado yana mashiko hata sasa hivi. Tunataka kuangalia iwapo mwanamke atarudi kupata ule usawa na uhuru aliokuwa nao au ataendelea kudunishwa na wenye nguvu ambao ni wanaume.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Tumetumia tamthilia mbili ambazo ni *Kilio Cha Haki* (1981) Alamin Mazrui na *Pango* (2003) K.W. Wamitila katika kulishughulikia swala la taswira ya mwanamke. Hiki kitakuwa chanzo cha kutaka kujua ikiwa mwanamke wa kisasa amefikia hali ya kujikomboa katika ulimwengu wa sasa.

Swala la taswira ya mwanamke japo limeangaziwa na wengi kwa njia hasi utafiti wetu umeshughulikia taswira ya mwanamke kwa njia mbili ambazo ni chanya na hasi, na uwezo anaotumia mwanamke kujikomboa.Tumeangazia majukumu mbalimbali ambayo mwanamke amepewa katika tamthilia hizi mbili.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kutathmini taswira ya mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili.Mwanamke anamulikwa na jamii na kupewa taswira ambayo haistahili. Tumeangazia yafuatayo: Ukombozi wa mwanamke na jinsi anavyoelekea kuikomboa jamii nzima, wanawake walio na mtazamo thabiti kuhusu mageuzi, wanawake waliokandamizwa na utamaduni kiasi cha kutoenda kinyume na utamaduni huo, mikakati aliyowekewa mwanamke na jamii na mwelekeo wa mwandishi kuhusu ukombozi wa mwanamke.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umechunguza nadharia tete zifuatazo;

1. Kaida alizowekewa mwanamke na jamii katika *Kilio Cha Haki* na *Pango* zinaathiri uwezo wake wa kujikomboa
2. Wahusika wa kike wanazidi kudhulumiwa na jamii.
3. Waandishi wa tamthilia hizi wametambua juhudi mbalimbali zinazofanywa na wanawake katika kutafuta ukombozi wao na ule wa jamii kwa jumla.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Tamthilia za hapo awali hazikummulika mwanamke na kumpa majukumu yanayomfaa katika jamii, lakini tamthilia za sasa hivi ambazo tumezitathmini zimetambua juhudi za mwanamke katika jamii na kumpa majukumu muhimu ayatekeleze. Kulingana na tamthilia tulizozishughulikia swala la taswira ya mwanamke limejitokeza bayana na linadhihirika wazi.

Katika mataifa mengi wanawake wamepewa haki na usawa kisheria lakini hawawezi kutekeleza kwa sababu ya uwezo mdogo walionao.Tumetathmini ikiwa mwanamke anaweza kujikomboa kupitia kwa kipawa chake cha kuzungumza bila uwoga wowote ili aikomboe jamii. Kwa vile tamthilia inahusisha mazungumzo na utendaji taswira ya mwanamke inajitokeza vizuri.

Kazi tulizozichagua ingawa ni za wanaume tumeziteua ili tuitathmini sauti waliyompa mwanamke. Waandishi hawa wanaweza kuwa wamempa mwanamke sauti chanya tofauti

na kazi za awali zilizompa mwanamke sauti hasi na hata kumpuuza. Katika kazi tulizoziangalia, mwanamke amemulikwa na kupewa nafasi kubwa hata ya uongozi na nafasi hii inamwongoza mwanamke kuikomboa jamii nzima. Tafiti za awali zimemwangalia mwanamke kihasi. Je! Katika kazi hizo kuna mahali popote nguvu za ukombozi wa mwanamke zinaonekana.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti wetu ulijikita katika tamthilia za *Kilio Cha Haki* (1981) na *Pango* (2003). Tumeangazia matatizo ya mwanamke yanayotokana na mitazamo ya jamii. Udhalimu huu umeendelezwa na, viongozi katika jamii na jamii yote kwa jumla wakiwemo pia wanawake.

Katika kuangalia kazi hii tumerejelea kazi nyingine zinazoshughulikia taswira ya mwanamke ili kutilia mkazo hoja fulani katika kazi zetu. Tumeangalia mitazamo mbalimbali anayopewa mwanamke na jamii, nafasi walizonazo wanawake za kuzalisha mali na ikiwa nafasi hizo zinawafaa kwa njia yoyote ile katika harakati za kupigania haki zao.

Tumeangalia mitazamo ya wanaume katika ngazi mbalimbali kuhusu mwanamke. Wananadharia mbalimbali wamechangia swala la kudhalilishwa kwa wanawake lakini ni bayana kwamba wanajitokeza na mikakati anuwai ya kukabaliana na matatizo ya wanawake.

Tumeangazia njia mbalimbali ambazo viongozi hawa wanatumia kumkandamiza huyu mwanamke, majukumu ya mwanamke katika jamii na uwezo wake wa kuzalisha mali katika jamii. Na je, akiwa na huo uwezo, anaweza kujikomboa kutokana na udhalilishaji wake na mwanamume au atabaki tu kudhulumiwa. Tumeangazia pia uhusiano ulioko kati ya mwanamke na wanaume wengine katika jamii. Katika tamthilia ya *Pango* tumeangazia mitazamo mbalimbali ya viongozi kuhusu mwanamke, hususan viongozi wa kiume katika jamii na jinsi wanavyomwangalia mwanamke katika harakati zake za kutaka uongozi.

Katika *Kilio Cha Haki*, tumeangalia dhuluma zinazomkumba mwanamke katika harakati za kuokoa jamii na jinsi anavyopigana na dhuluma zidi yake na jamii kwa jumla. Tumeangazia nafasi walizonazo wanawake za kuzalisha mali na ikiwa zitawafaa katika harakati za kupigania haki zao.

**1.7 Msingi wa Nadharia**

Nadharia tuliyotumia katika utafiti huu ni ya ufeministi wa Kiafrika. Hii ni nadharia inayoangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume na kuwa shida zinazowakumba hujengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Hujaribu kufichukua matatizo yawapatao wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake.

Wamitila (2000) anaeleza kuwa ndoa ni asasi mojawapo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake. Anasema asasi kama dini inatilia mkazo au nguvu itikadi

ya kiume inayopatikana katika jamii nyingi.Asasi hii inaishia kuzipa nguvu mpya tamaduni dhalilishi dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya maamko ya kidini.Wamitila anazidi kusema kuwa uhakiki wa ufeministi ulishika nguvu katika karne ya kumi na tisa na kuendelea kukua na kuanza kutia fora miaka ya sitini na sabini. Hata hivyo anaelezea kuwa hii haina maana kuwa hapakuweko na kazi zilizomulika na kuliangazia swala la haki na ukombozi wa mwanamke.

Mbatiah (2001:87) anaeleza ufeministi ni nadharia ya kifasihi ambayo inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii yenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume.

Haya yanabainishwa na Wafula na Njogu (2007:90). Anapoeleza kwamba athari ya ufeministi msingi wake mkubwa ni kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Waasisi wa Ufeministi walikuwa na lengo la kuwaunganisha wanawake ili wajipiganie kama kundi moja. Wakilenga kujikomboa kwa kuzua taswira chukivu kwa mwanamume ambaye alipaswa kuchukuliwa kama adui mkubwa.Vipengele tutakavyovitumia katika utafiti huu ni vile ambavyo vinashikilia kuwa nadharia hii inaeleza kuwa uhusiano uliopo kati ya wanaume na wanawake unaonyesha dhuluma kwa mwanamke.

Wahusika wa kike wamesawiriwa kwa njia hasi na kuegemezwa kwa wenzao wa kiume na mkabala walionao wahusika wa kiume kuwahusu wahusika wa kike ni hasi. Kulingana

na nadharia hii twaona kuwa haki zote ambazo mwanamume amepewa, mwanamke, amenyimwa na hakuna sababu zozote zinazotolewa.

Teneti tutakazo zitumia katika utafiti huu ni kuwa.

1. Ufeministi wa Kiafrika unatambua uhusiano wake na ufeministi wa Kimagharibi, lakini unafafanua ufeministi ambao mahitaji na malengo maalum yanatokana na uhalisi wa maisha ya wanawake katika jamii za kiafrika
2. Unatambua kihistoria kuwa katika jamii ya kiafrika kabla ya ukoloni kulikuwa na watawala na mashujaa wanawake.
3. Unaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na kupuuza unyanyasaji na utumwa unaomkabili.
4. Unachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi wa kitaifa na ujenzi wa jamii mpya.

Ufeminisiti wa Kiafrika umeibuka kutokana na madai kuwa mitazamo ya ufeministi wa kimagharibu haitoshelezi udadisi wa hali zisizokuwa na usawa hususan za kiuana. Katika jamii ya Kiafrika kunahitajika mitazamo ya Kiafrika ambayo itahakiki tajriba za wanawake wa Kiafrika kutegemea mifumo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa katika jamii husika.

Ufeministi wa Kiafrika unaingiana na wa Kimagharibi pale ambapo mitazamo yote inatambua maswala ya uana na kuelewa nafasi ya kimataifa ya mwanamke. Popote pale mwanamke ni mwanachama wa kiwango cha chini na ipo haja ya kuirekebisha hali hii

Mwasisi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika anaaminiwa kuwa ni Steady. Aliliangalia swala la mwanamke kwa mapana. Mwanamke anawakilisha sehemu kubwa ya jamii ambayo imedhulumiwa na wenye nguvu, kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika tunaaelewa chanzo cha kukandamizwa kwa mwanamke katika jamii.Nadharia hii hutusaidia kutatua matatizo ya mwanamke pale mwanamke anapojikomboa. Wanawake huchangia sana katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa na utawala mwingi umeelekezwa kwa mwanamume na kumsahau mwanamke.

Kulingana na Ramazanoglu. C. (1989) katika *Feminism and The contradictions of Oppression.* Anaeleza kuwa historia ya Ufeministi wa Kiafrika ilianza kuwaathiri wanawake kuanzia miaka ya sitini. Ilianza na wanawake ambao walikuwa wakidhulumiwa. Wanawake hawa walieleza kwa ujumla kwamba wanawake wana mahitaji tofauti na yale ya wanaume. Wanaendelea kusema kwamba wanaume huwakandamiza wanawake na kwa ujumla wanaume hufaidi kutokana na dhuluma hii.Wanaendelea kusema kuwa katika mwaka wa 1970 wanaharakati wa Ufeministi walianza kusisitiza tofauti zilizokuwa kati ya wanawake. Wakati mmoja umakinifu ulisisitizwa kuhusu tajriba ya wanawake, na uwezo wa wanawake dhidi ya wanawake wenzao na nguvu za siasa na uchumi zilizomilikiwa na wanaume na wanawake.Wakati huu ndipo matatizo ya ufeministi yalipozuka. Wanaendelea kusema kwamba ikiwa wanawake hawana mahitaji yanayofanana hivyo basi hakuna vile ufeministi unaweza kuboresha maisha ya wanawake.

### 1.7.1 Mirengo ya Ufeministi

#### (a) Ufeministi huru:

Hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Wakati mwingine ufeministi huu huitwa ufeministi wa kibepari. Mkondo huu hushikilia kwamba maadamu wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote wake kwa waume wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu na malengo yao.

#### (b) Ufeministi wa Kiharakati:

Huu humchukua mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Waitifaki wa mkondo huu wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanaume kumkandamiza na kumdhalilisha. Kwa hivyo, ili wanawake' waweze kujitawala katika nyanja zote za maisha wanahimizwa wasiolewe na wanaume. Kinyume na haya wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi.

#### c) Ufeministi wa Kijamaa:

Ufeministi wa kijamaa hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa uwezo mwenye kumiliki njia kuu za kuzalisha mali kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka na unyonyaji katika misingi ya kijinsia. Ufeministi wa kijamaa unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake.

### 1.8 Yaliyoandikwa juu ya mada.

Baadhi ya kazi za mwanzomwanzo kuyafafanua maswala ya mwanamke kinadharia zilikuwa za Aristotle (1888) alieleza kwamba maishani wanawake huwa chini ya utawala wa wanaume. Utotoni wanajinyenyekea kwa baba zao na wanapoolewa hujinyenyekea kwa waume wao. Hali hii ndiyo inayozingatiwa na jamii za Kiafrika.

Kazi nyingine iliyofafanua maswala ya mwanamke ni A *Vindication of the Rights of Women* (Mary Wollstonecraft, 1729). Alidai kwamba mielekeo hasi kumhusu mwanamke imesababishwa na elimu mbovu wanayopewa wanawake na wanaume. Kwa mujibu wa wahakiki wa kifeministi kama Birk (1986) na Lovenduski na Randall (1993) ufeministi ni dhana inayoeleza hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume. Katika utafiti wetu nadharia ya ufeministi wa Kiafrika itatufaa sana. Kwa sababu tunamshughulikia mwanamke wa Kiafrika.

Kathleen. N. (1979) katika *The Sisterhood of Man* anaeleza kuwa kitamaduni, majukumu ya jinsia mbili katika familia ni changamoto kubwa kwa wanawake wakati wanapopigania usawa.Anaendelea kusema kwamba mtoto msichana anapozaliwa anakuwa sikitiko kwa wazazi wengi. Zaidi ya hayo msichana anadhaminiwa kwa kulingana na mahari atakayopewa mzazi wake na uzao atakaokuwa nao. Anazidi kusema kuwa ingawa wanawake wamefaulu kidogo kupata usawa bado hawana uwezo mkubwa wa kujikomboa na maendeleo hayaonekani yakipiga hatua.

Caroline B. (1947) katika *Gender in Cross Cultural Perspectives* anasema kwamba mwanamume na mwanamke wako tofauti kimaumbile. Majukumu waliyopewa wanawake na wanaume kiutamaduni yalichukuliwa kuwa yalihusiana kulingana na viungo vya binadamu. Katika miaka ya (1930-1960) utafiti wa tamaduni tofauti kuhusu ugavi wa kazi ulionyesha wanawake na wanaume walishindwa kutekeleza kazi walizopewa.

Freire P. (1972) katika *The Pedagogy of the Oppressed* anasema kwamba uhuru hupatikana kwa kujipigania wala sio kwa hidaya. Hakuna awezaye kuelewa umuhimu wa ukombozi isipokuwa yule anayetawaliwa. Hivyo ukombozi hauna budi utokane na hao walionyanyaswa. Utafiti huu utatusaidia kwa kuwa tunaangalia njia mbalimbali ambazo mwanamke anatumia ili kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume.

Martin, A. (1975) katika Women *and Imperialism* anasema kwamba wanamageuzi wa kike kule Kanada wanachanganua kwa utaratibu vile wanawake wameathiriwa na utendakazi wa kibepari ulimwenguni kuanzia karne ya kumi na tisa hadi sasa.

Carr S. (1975:2-6) anazungumzia kuhusu ubaguzi wa kijinsia ulimwenguni kote na anasema kwamba juhudi zinafanywa na vyama vya miungano ya wafanyikazi ili kufutilia mbali ubaguzi huo.

Spender .D. katika chapisho la *Man Made Language* (1980:3) Anaelezwa kuwa lugha hueleza au huonyesha mipaka ya mawazo yetu, na hivyo ulimwengu wetu. Maana

yanayobebwa na maneno huundwa na utamaduni wetu. Kwa hivyo matumizi ya 'uume' na 'uke' kuweka pamoja mwanamume na mwanamke si makosa na mapatano ya mwanaisimu lakini hutupa ujumbe kuwa katika jamii zetu wanaume siyo ajali kuwa wanadhaminiwa kuliko wanawake lakini hao wako hivyo kwa sababu jamii imewatukuza kuliko wanawake na inawataka wawe hivyo.

Croll E. J. (1982: 26-37) anaeleza kwamba wanawake wanafaa kupewa uhuru wa kiuchumi kwa kuondoa ruwaza ya nguvu za ubabedume. Anaendelea kusema kuwa ingawa wanawake waliahidiwa msaada kutoka kwa nchi zao ili kupunguza kazi za nyumbani, wanawake bado wanafanya kazi maradufu za nyumbani na mahali wanapoajiriwa huku wakilipwa mshahara wa chini sana.

Jaquettee, J. S. (1982: 267-284) anajadili maandishi mbalimbali kuhusu majukumu ya wanawake katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa na matokeo ya sheria za maendeleo kwa wanawake, anazidi kuongea kuhusu michakato ya usasa na mahusiano yaliyoko kati ya uhusiano wa mwanamume na mwanamke. Kazi hii imetufaa kwa kuwa tumeshughulikia majukumu ya mwanamke katika jamii.

Dahli (1982) Anaeleza kuwa mwanamke anafunzwa na kukuzwa akijua kwamba jukumu lake ni jikoni ambapo anahitajika kutunza nyumba watoto na mumewe. Kazi hii imekuwa na manufaa kwetu kwa sababu tumechunguza majukumu ya mwanamke katika jamii licha ya kuwa anapewa mtazamo hasi na viongozi wa kiume.

Mugambi P.M. (1982) Alishugulikia *Maudhui Katika tamthilia za Kiswahili zililzo*chapishwa*(1957-1982).* Anasema kwamba mwanamke amebanwa na kupewa sifa za mnyonge asiye na nguvu na wala uwezo mbele ya mwanamume lakini anajaribu kupinga hali hii duni. Kulingana na maelezo haya ukombozi wa mwanamke utapatikana tu ikiwa mwanamke mwenyewe ataiondoa sifa ambayo amepachikwa kuwa yeye ni mnyonge na ajione kuwa yeye ni binadamu kamili kama mume na ni binadamu aliye na uwezo wa kujiendeleza .Mugambi alishughulikia maudhui hasi kumhusu mwananamke.Kwa kutumia nadharia ya Umaksi ameonyesha kwamba mwanamke anahitaji kukombolewa. Sisi tunatumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.Kazi hii imetusaidia kwa kuwa tumeangalia taswira ya mwanamke na njia anazotumia kujikomboa.Tumeonyesha kwamba mwanamke ana uwezo wa kujiondoa katika dhuluma ambapo yeye huonekana kama mnyonge.

Lugano (1989) Alishughulikia mwanamke katika riwaya za Kezilahabi. Kazi hii imemsawiri mwanamke kwa njia hasi na kuwa yeye ni chombo hasi cha kumfurahisha mwanamume. Lugano alitumia nadharia ya umaksi. Hajapendekeza njia ambazo mwanamke atazitumie kujikomboa kutokana na hali hii ya kudunishwa na mwanamume.Aliangazia jinsi mwanamke anavyoumbwa na kusawiriwa kisiasa, kiuchumi na kielimu. Anasema kwamba jukumu muhimu ambalo amepewa mwanamke ni lile la uzazi. Jukumu hili linapewa umuhimu mkubwa sana kiasi cha kumfanya mwanamke mwenyewe kukubali kuwa hakuna jambo lolote linalomfaa isipokuwa kuolewa na kuzaa watoto.

Lugano anaendelea kusema kuwa wanawake wengi wanaharibu muda wao mwingi wakijaribu kujirembesha ili kuwafurahisha waume zao, badala ya kujishughulisha na shughuli za kuboresha maisha yao. Anasema kuwa asasi ya ndoa inaonekana kuwa mojawapo ya mbinu zinazotumiwa kumfanya mwanamke kuwa mtumwa wa mwanamume. Utafiti huu ijapokuwa ni wa riwaya, umetufaa sana kwa sababu sisi tunaangalia taswira ya mwanamke katika jamii kutokana na majukumu aliyotwikwa na jinsi anatumia uwezo wake kujikomboa.

Kiango (1992) katika tasnifu yake ameangalia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. ameihakiki tamthilia ya *Kilio Cha Haki* na kusema kuwa inastahili kupewa nafasi ya kipekee kwa sababu mkabala wa Mazrui ni tofauti na waandishi wengine. Katika kazi nyingi za fasihi mwanamke amechorwa kama mtu ambaye hana usawa na mwanamume na pia kitega uchumi, mbaya, mzinifu, muuaji, mshirikina n.k kazi hii imetufaa sana katika kuendeleza swala la mtazamo hasi aliopewa mwanamke.

Dhahabu (1994), alishughulikia uumbaji na ueendelezaji wa mhusika mwanamke katika tamthilia nne za Penina Muhando. Dhahabu alishughulikia swala la fani tofauti na sisi tunaoshughulikia taswira ya mwanamke. Kazi hii itatusaidia kwa kuwa ni kupitia kwa fani ambapo tutaona picha halisi ya mwanamke.

Momanyi (2001) alishughulikia nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Alijikita katika swala la matumizi ya lugha. Alibainisha taswira ya mwanamke kama pambo, kifaa cha mwanaume, asiyeaminika na anayenyekea katika matumizi ya lugha.

Kazi hii imetufaa kwa kuwa tumeangazia jinsi mwanamke anaweza kujinasua kutoka kwa dhuluma ya mwanamume kupitia usemi wake mwenyewe.

Maina (2005) alishughulikia nafasi ya mwanamke katika *Tenzi za: Shaaban Robert Utenzi wa Hati na utenzi wa Adili.* Kazi hii imetufaidi kwa kuwa tumeangalia na kuchunguza vipengele vya kiuchumi, kisiasa na jamii vinavyochangia katika kumtweza mwanamke. Utafiti huu ulishughulikia riwaya, tofauti na utafiti wetu ambao utashughulikia Tamthilia.

Simone De Beauvoir (1949) katika kazi yake iitwayo *The Second Sex,* anaonyesha jinsi mwanamke alivyodunishwa katika asasi ya ndoa. Mwanamke anachukuliwa kama msaidizi wa mwanamume licha ya kuwa yeye ni binadamu kama mwanamume. Anaendelea kusema kwamba mwanamke ni kama bidhaa machoni mwa mume, akiwa mtoto anamilikiwa na babake na anapokuwa mkubwa babake humwoza kwa mwanamume mwingine ambaye humfunga katika pingu za utamaduni zinazomfanya mwanamke kukubali kudhalilishwa.

Kutokana na fafanuzi hizi ni bayana kuwa Ufeministi wa Kiafrika na Ufeministi wa Kimagharibi unalingana unapomzungumzia mwanamke kijumla lakini tofauti zinapatikana pale unapomwangalia mwanamke kindani.

Katika utafiti wetu tunaamini mwanamke anayo nyenzo mwafaka kabisa katika kujikomboa.Kutokana na yale ambayo tumeyasoma kuhusu kudunishwa kwa mwanamke

kupitia ubabedume tunaona kwamba njia mojawapo ya kujikomboa kwa mwanamke ni kupitia kwa kipawa chake cha kuzungumza.

## 1.9 Njia za utafiti

Utafiti wetu ulikuwa maktabani. Tumesoma kazi ambazo zimeandikwa kuhusu *Kilio Cha Haki* na *Pango*. Tumesoma pia tamthilia *zinazomulika* mitazamo mbalimbali ya viongozi kuhusu wanawake . Tumesoma vitabu vilivyo na maelezo kuhusu nadharia tuliyoitumia katika utafiti huu. Tumefanya utafiti kutoka kwenye Tovuti. Mara kwa mara tulipata msaada kutoka kwa wataalam wa fasihi.

## SURA YA PILI

## 2.0 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA *KILIO CHA HAKI (1981)*

### 2.1 Utangulizi

*Kilio Cha Haki* ni tamthilia ya mapambano baina ya wafanyakazi na udhalimu wa Makaburu walioivamia nchi yao. Wafanyikazi hao wanaongozwa na mwanamke jasiri aliyejikomboa kimawazo, ambaye anadhihirisha udhalimu wa jumuiya yake unaowapata kuwazindua wafanyikazi wenzake wapambane na udhalimu na waweze kutetea haki zao. Kuhamasishwa huku kunaleta mwamko wa kisiasa ambao ndio mwanzo wa matayarisho ya vita vilivyoikomboa nchi nzima kutokana na ukoloni.

Katika harakati hizi Lanina anapitia mambo mengi magumu yakiwemo kutiwa kuzuizini kwa kosa la kuwachochea wafanyikazi. Akiwa kule kuzuizini anateswa sana na askari ambao wanampiga na hata kujaribu kumbaka. Anatusiwa na askari na hata kuitwa majina mengi kama malaya. Lanina hajali haya yote. Hata anapoelezwa na askari kuwa Tereki alikuwa amekubali kuachana na mambo ya mgomo na kurudishwa kazini, anashagaa sana jinsi Tereki alivyowasaliti wafanyikazi wenzake. Anakata shauri kutowasaliti wenzake.

Lanina anakataliwa na mzazi wake wa kiume bwana Seromanga.Seromanga anamkana Lanina na kumkataza kuwa asimwite 'baba' kwa kuwa yeye hakuzaa malaya. Mume wake Lanina anawalalamikia wazazi wa Lanina kuhusu mwenendo wa mwanao. Anasema kwamba tangu Lanina ajiingiza katika siasa za wafanyikazi, hamjui tena. Alikuwa amechoka na minong'ono ya watu kumhusu Lanina. Lanina alikuwa anapigania hali nzuri ya kazi kwa wafanyikazi wote. Jambo lililomwingiza katika matatizo.

### 2.1.1 Mwanamke kama binadamu asiyezingatia maadili

Mwanamke anachukuliwa kama binadamu asiye na maadili mema hasa pale anapokosa kukubaliana na wanaume kulingana na msimamo wake.Lanina anatusiwa kuwa yeye ni malaya na baba yake na hata na mume wake Mwengo.Anapotembelewa na wafanyakazi wenzake, Mwengo anampiga kwa kumsingizia kuwa amewaleta wanaume katika nyumba yake. Mazungumzo yafuatayo yanaashiria jinsi Lanina alivyokosa maadili kulingana na babake na mume wake Lanina, Mwengo:

LANINA: *(Kwa Kustaajabu)* Babaa!.....

BABA: Nimekwambia usiniite baba, husikii?

Ndiyo! Mimi sikuzaa malaya!

Wala sikuzaa wana wasaliti!

Ndiyo! Sikuzaa binti yeyote anayeweza kuisaliti nchi yake

Sikuzaa binti anayetaka uume!

Hee-he! Mimi Seromanga!

Mimi! Mimi! Nizae mke-mume!

Heee-he! Labda mtu mwingine;

Si mimi.

MWENGO: Lanina! Si nimekwambia sitaki wanaume hapa! *(Anawasogelea)* nyinyi washenzi, mtanitambua leo;

LANINA: Wacha ujinga Mwengo….

MWENGO: Ujinga siyo! Basi leo…utauona ujinga wangu. Mambo nimeyaona mwenyewe leo…kwa macho yangu.

Unafikiri mimi…mimi si mume,

Siyo? Basi utaujua udume wangu leo malaya wewe!

Tereki, Matovu na Peleka wanapoenda kumtembelea Lanina kwa kioski cha mzee Ingeli wanakutana huko na wateja wawili ambao wamefika ili kunywa uji. Katika mazungumzo yao wanaonyesha jinsi wanavyomchukulia mwanamke. Wanamtania Lanina na kusema:

| | |
|---|---|
| MTU WA 1: | Naona umetuletea kipusa, babu. Biashara yako sasa<br>Umeitia ladha kweli kweli. |
| LANINA: | Habari zenu ndugu<br>Uji au chai? |
| MTU WA 2: | Na wewe mwenyewe je?<br>Mbona umejitoa katika orodha dada? |
| LANINA: | *(akicheka)* Siuzwi wala siuziki kaka? |
| MTU WA 3: | *(Akipiga kofi kidogo na kucheka)*<br>Hapo umesema dada!<br>Huuzwi wala huuziki!<br>Lakini je mapenzi dada!<br>Mtu kama mimi naweza kukupenda sana.<br>Unasemaje dada!<br>*(Anamshika Lanina mkono na kijaribu kumvuta)* |
| LANINA: | Nina mume wangu bwana, Usinisumbue |
| MTU: | Si neno dada! Hata mimi nina mke, tena wawili (*akionyesha kwa vidole wenzake wawili wanacheka (uk. 57-58).* |

Kulingana na mazungumzo haya tunaona jinsi wanaume wanavyomdharau na kumdhalilisha mwanamke. Lanina anapowauliza kama awaandalie chai au uji mtu wa pili

anamwuliza sababu ya kijitoa kwenye orodha ya menyu. Mwanamke anafananishwa na chakula. Ni kwamba thamani yake ni kama ya chakula kinachouzwa. Hata Lanina anaposema hauzwi wala hauziki, dharau zinamwandama. Anachukuliwa kama chombo tu cha kutimiza haja za mwanamume hata kama amęolewa. Hii ina maanisha kuwa baadhi ya wanaume hawaziheshimu ndoa zao.

Askari anamwendea Lanina kwa azma ya kumsaidia lakini kupitia njia sizizo halali. Anamwambia kuwa atamsaidia akimruhusu wafanye mapenzi. Haya yanadhihrika kupitia kwa matamshi ya askari kule gerezani.

ASKARI: Sasa dada…unajua…mimi…nataka kukusaidia…unasemaje? *(kimya)* yaani wewe tunaweza kuona raha, na mimi nitakusaidia. Nitakuletea chakula kingi, sigara na mambo namna hii. Unasemaje dada? *(Anamsogelea tena).*

LANINA: Tafadhali toka!

*(Askari anamsogelea, Lanina anarudi kinyumenyume)*

ASKARI: Sasa unataka kujifanya mkaidi siyo? Haya basi tutaonyeshana!

Askari anamdharau Lanina. Anaona kuwa mwanamke ni mwepesi sana kukubali unyama wa mwanaume kwa kuwa malipo baada ya kufanya naye mapenzi ni chakula na sigara. Anakosa kutambua kuwa mwanamke anastahili kuheshimiwa kama binadamu mwenzake. Lanina anakabaliana na huyo askari hasa pale anapomrukia na kujaribu kumbusu na kumpasulia nguo. Lanina kwa kujitetea anampiga goti kwenye sehemu zake za chini. Askari anaanguka chini na kuanza kulia kwa maumivu.

Kachero wa kwanza ana mtazamo huu unaomdunisha mwanamke, anamshika Lanina kidevu, usoni, mabegani na kwenye mashavu. Anamwambia Lanina kuwa haikuwa na haja kujiumiza na kijichafua bure kwani alikuwa mwanamke mrembo sana.(Uk 22).

Mwanamke anakumbana na dhuluma za kimapenzi kwa kuchukuliwa kuwa yeye ni chombo cha kutimizia haja za mwanamume kimapenzi. Lanina anadhihakiwa na kudharauliwa na wanaume wateja kwenye kioski cha Mzee Ingeli.

Kachero wa I anamwona Lanina kama mwanamke asiye na maadili na anatafuta mbinu ya kumfanya Lanina ampende kwa lazima  Anapeleka mikono yake na kuanza kumpapasa Lanina. Lanina anashikwa  na hasira na kumwambia Kachero kuwa asimfanyie uhuni huo kwa kuwa yeye hakuwa malaya.  Kachero anakasirika na anampiga Lanina kofi linalomwangusha chini. Kachero anasema:

KACHERO WA 1: Niwache Bunda, Niwache! Mwanamke hajapata kunitusi namna hii. Mimi mhuni! Mhuni! Malaya huyu nitamwonyesha leo! (uk.25)

KACHERO WA 1: Huyu mwanamke gani huyu? Anamwacha mumewe na watoto nyumbani huku akizurura na wanaume wengine, ati wanapigania haki zao. Haki gani? Labda haki za umalaya! Labda…

Baba yake Lanina anaonyesha ubabedume kwa kujipiga kifua na kusema kuwa yeye ndiye dume na hataki kuhusishwa na Lanina kwa kuwa Lanina hana tabia za uke. Kwanza yeye ni malaya na hataki kuhusishwa na mtoto malaya. Pili, Lanina anataka kuwa mume kwa kushiriki siasa.

Friedman katika Gaskof (1963) Anaeleza kuwa wanawake katika jamii nyingi wananyanyaswa kupitia kwa vyombo vya habari ambapo wanaonekana wakiwashawishi watu kununua bidhaa wanazouza kama chakula cha mbwa, magari tarakilishi na manukato.Friedman anasema kuwa ikiwa utanunua kifaa kinachouzwa, utazidisha nafasi ya kupata kifaa kingine ambacho ni mwanamke.

### 2.1.2 Mwanamke kama kiumbe asiye na mielekeo inayofaa

Mwanamke anachukuliwa kama kiumbe asiye na mielekeo inayofaa anapojiingiza katika siasa za kutetea haki za wafanyakazi. Siasa hizi zinachukuliwa kama uchochezi unaosababisha mgomo.

Haya yanabainika wakati Musa na Dewe wanapokutana kisha Dewe anasema kuwa amepata habari fulani kuhusu Lanina. Kulingana na maelezo ya Bwana Delamon, kwa Kamishena wa polisi, uchochezi wa Lanina ndio uliosababisha mgomo. Tazama anavyoeleza Dewe:

DEWE: Haya *(anaanza kusoma kwa kusitasita)* "Lanina Kupelekwa mahakamani. Lanina wa Muyaka, mwanamke aliyekuwa mfanyikazi katika shamba maarufu la Bwana Delamon, ametiwa tena kizuizini.

Kamishena mkuu wa polisi, Bwana Handerson, alisema kwamba Lanina alichochea mgomo mkubwa wa wafanyikazi wa shamba la bwana Delamon tarehe 1 Mei, uliosababisha mauaji ya manakoa watatu wa shamba hilo….." (uk. wa 2).

Lawama hii ya inaendelezwa pia na askari anaposema:

ASKARI: Mmekamatwa kwa hatia ya kuchochea mgomo .Mna lolote la kusema kabla hatujakupelekeni ndani.

SHINDO: Lanina si mtu wa busara.Siasa zake ni za kuchochea tu.Hatuwezi kufanya kazi na mtu aina hiyo.

Vilevile Lanina anachukuliwa kama muuaji. Hii inabainika kutokana na maelezo ya Bwana Kamishena Henderson. Inaonekana kuwa wakati wa mgomo Lanina hakuwepo. Mgomo huo ulipofanyika kuna mauaji yaliyotokea. Bwana Delamon Shindo na Tereki waliuawa. Kamishena alisisitiza kuwa ingawa Lanina hakuwepo wakati huo wa mauaji yeye ndiye aliyechochea mgomo huo wa kikatili. Kulingana na maelezo ya bwana Kamishena Hernderson, amechukulia kuwa uchochezi ndio ulioleta mauaji na kwa hivyo mauaji hayo ni mpango wa Lanina Tazama yafuatayo:

WAKILI: Naam…Lanina wa Muyaka, mashtaka yako yanahusu mauaji.

LANINA: (*akistaajabu*) Mauaji? Mauaji ya nani?

WAKILI: Mauaji ya Bw. Delamon, Bw. Shindo na rafiki yako mwenyewe Bw. Tereki.

KACHERO: Wewe ni mshirika katika mauaji hayo Lanina.

DEWE: Haya (*anaendelea kusoma)*

"….yeye ndiye aliyechochea mgomo wa kikatili. Kwa hivyo atapelekwa mahakamani karibu kwa mashtaka ya kushiriki katika mauaji hayo…"

Dhuluma ya mauaji ilitendwa na wanaume ilhali Lanina analaumiwa kwa kosa ambalo hakulitenda.

Ubaguzi huu wa kijinsia umeelezwa na Carr Shirley (1975) ambaye anaeleza kuwa kun hatua zinazofanywa na vyama vya muungano wa wafanyikazi ili kufutilia mbali ubaguzi huo.

### 2.1.3 Mwanamke kama kiumbe dhalili

Mwanamke amechorwa kama kiumbe dhalili pale ambapo anashindwa kujitetea kulingana na dhuluma dhidi yake.Katika *Kilio Cha Haki* kuna mwanamke aliyeshambuliwa na majibwa na hakuwa na mtu yeyote wa kumtetea.

Kulingana na sheria ya kibeberu, haikuwekwa kulinda au kutekeleza haki. Sheria hiyo ilikuwa ya kuwalinda wanyonyaji na mali yao. Sheria hii iliwawezesha kuendeleza unyonyaji na udhalimu kwa Waafrika na hasa Waafrika wanyonge. Dewe anasema:

DEWE: Hiyo ndiyo sheria ya kibeberu. Haikuwekwa kulinda na kutekeleza haki! La! Imewekwa kuwalinda wanyonyaji kulinda rasilmali Yao. Na kuendeleza udhalimu wao. Si unakumbuka ile kesi ya yule msichana wa kishamba. Aliyetafunwatafunwa na majibwa ya bwana shamba. Ati kwa sababu alipitia katika Shamba lake! Bwana shamba huyo amefanywa nini mpaka leo? Anaendelea kuishi raha mstarehe ilhali wazazi wa msichana wanasononeka kwa maumivu ya dhuluma waliyotendewa. Hiyo ndiyo sheria ya kibepari Musa. Sheria ya mwenye nguvu mpishe!

MUSA: Sheria ya kibeberu!

Sheria ya kuua haki!

Kwa nini iheshimiwe!

Shenzi! (*Anatema mate tena*) kimya

Bwana Delamon akiwa ofisini kwake pamoja na wasaidizi wake, Zari na Shindo anasikia sauti kutoka kwa wafanyikazi waliogoma. Anapouliza wasaidizi wake wanamwambia ni sauti za watu wachache tu. Zari anajibu kwa kusema kuwa ni yule Lanina tu … Yule mshenzi. Kulingana na Zari hakumwona Lanina kama mtu aliyekuwa akiongea ukweli fulani. Aliona yeye ni mshenzi na mawazo yake yalikuwa ya kishenzi. Haya pia yanaungwa mkono na Delamon anaposema:

DELAMON: Mwanamke? Yaani mzozo wote huu ni kazi ya mwanamke. Mwanamke mmoja tu? Naye amewashinda? Hamkuweza kumnyoosha? Nimefanya ujinga ulioje kuwapa kazi madubu kama nyinyi! (uk 8)

Hii ni taasubi ya kiume inayoendelezwa na Delamon. Ni taasubi isiyokubali ukweli kwamba mwanamke ana kipawa na maarifa na anaweza kuwaongoza watu haswa wafanyikazi katika kutetea haki zao.

Kulingana na mawazo ya Delamon anamwona Lanina kuwa "mwanamke tu". Kumaanisha mwanamke kimaumbile ni mtu myonge na hawezi lolote. Yuko kila wakati chini ya mamlaka ya mwanamume. Mwanaume yu huru kumtendea mwanamke lolote hata kama ni kumdhuru. Ndio maana anasema kuwa "hamkuweza kumnyoosha?"

Delamon ana taasubi za kiume na anaendeleza ubabedume kwa kusema kuwa mwanamke anakomeshwa kwa kunyooshwa. Kunyoosha kuna maana ya kumpiga mwanamke. Delamon anakosa kujua kwamba ingawa Lanina ni mwanamke mmoja tu

anavyodai, anawakilisha jamii kubwa katika *Kilio Cha Haki.* Anataka kukomesha udhalimu wa Bwana Delamon kwa wafanyikazi wote. Hali yao ya kazi haikuwa ya kurithisha. Akawa anapinga kufanyishwa kazi kwa muda mwingi huku wakilipwa mishahara duni. Kwa hivyo alikuwa anapigania jamii nzima

Unyonge wa mwanamke umeangaziwa na Simon De Beauvoir (1949) katika *The Second Sex*.Anaeleza kuwa mwanamke hukandamizwa na tamaduni zinazomfanya kuonekana mnyonge na kukubali kudhalilishwa na kisha kutumiwa kuendeleza tamaduni hizo hasi.

### 2.1.4 Mwanamke kama kiumbe aliyekandamizwa na utamaduni

Mwanamke amekandamizwa sana na utamaduni katika ***Kilio Cha Haki***. Katika tamthilia hii mwanamke anaonekeana kutokuwa na mamlaka ya kufutilia mbali utamaduni wao. Utamaduni huu umemtia pingu mwanamke na kumtawala. Haya yanadhihirika wakati Lanina aanapomjibu Mwengo kuhusu malezi ya watoto. Anasema:

LANINA (*Kwa hasira)* Utamaduni! Utamaduni! Utamaduni ni kitu gani

Mwengo! Kwa nini sisi tuwe watumwa wa utamaduni wetu *(Anamgeukia tena Mwengo).*

Mwengo….

Si sisi tuliofinyanga utamaduni

Si sisi tulioupa uhai utamaduni

Uhai wa kutuongoa?

Basi kwa nini tuuache utamaduni

Ututie pingu na fahamu zetu kututawalia,

Utupige pande na tabia yetu ya kuzingatia?

Kwa nini Mwengo!

Tuendelee kuufuata utamaduni

Hata uwapo makosani yakini?

(Uk 32)

Utamaduni pia umemdhalilisha mwanamke sana na haya yanabainika wakati Seromanga anapoghadhabika kwa sababu ya Lanina anasema.

BABA: vijana wa siku hizi! hee-he!

Na hasa vijana wa kike…

Wao ndio waliotia fora kabisa

Wengine wanataka kuwa wazungu

Wengine wanataka kuwa waume

Hee-he! Ole wao wanotupilia mila mbali.

BABA: Nani aliyezungumza habari za Lanina hapa! Mimi nimetaja vijana wa siku hizi. Kwani yeye pekee yake ndiye kijana wa siku hizi? Na hata yeye huyo mwanao. Kwa nini nisimlaani.Kwani mila zetu hazikutufunza kuwa kila kiovu hulaania, au sivyo?

Mama yake Lanina wanapoendelea kujadiliana kuhusu maisha ya Lanina na jinsi amebadilika inajitokeza kwamba Mwengo amewalalamikia wazazi wa Lanina kuhusu mwenendo wake. Haya yanajidhihirisha kutokana na matamshi ya mama yake Lanina.

MAMA: Lakini na mumeo je, Lanina!

Mwengo anasema siku nyingi hujipikia mwenyewe….

…mara nyingi awaoshe yeye watoto.

Mara nyingine asafishe yeye nyumba.

Mwananangu, sasa hivyo atakuwa ameoa au ameolewa? Si kuoa huko mama Mumeo apike, afagie, afue, eh? Si utakuwa umemwoa hivyo Lanina, badili ya yeye kukuoa wewe?

Mama yake Lanina anawakilisha wanawake ambao wamekandamizwa na mila na tamaduni lakini hawajui jinsi ya kujinasua kutokana na mila hizo. Anashikilia kuwa kazi yote ya nyumbani ni lazima ifanywe na mke.
Hii ndiyo njia moja ya kuonyesha unatii mila na tamaduni. Kwake anachukulia kwamba mume anaposhiriki upishi, usafi na kuwatunza watoto basi huyo mume ameolewa na mke, jambo ambalo si la kawaida kitamaduni.

Lanina anawakilisha mwanamke wa kisasa na anashikilia kuwa hizo ni mila za kuwafanya kuwa watumwa. Haoni ubaya wowote iwapo Mwengo ataihudumia familia yake. Lanina anapinga hali hii na kumwambia Mwengo kuwa utumwa wa kiutamaduni ni mbaya na kuwa asiuache utamaduni umtie pingu za kumtawala fahamu.

Kwa namna hii inamwelekeza Mwengo kufahamu kuwa kuitazama aila yake wakati Lanina hayupo si makosa. Wanawake wanapokuwa na kukulia katika jamii zao, wanayachukulia mawazo yanayoendeleza itikadi hasi na kwa njia hii kudharau jinsia yao

wenyewe. Hivyo utamaduni anamokulia mwanamke unamfanya aamini na akubali kuwa anapaswa kuikubali hali hiyo. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mamake Lanina amefungwa na pingu za utamaduni kutokana na jamii anamoishi na kuamini kwamba nafasi ya mwanamke ni jikoni.

Mama yake Lanina anamkumbusha kuwa tangu utotoni amefunzwa daima mke awe chini ya mume , kuwa lazima amtii anyenyekee na kumhudumia mumewe.Lanina hakubaliani na mamake na anasema:

LANINA: Lakini hayo si mambo ya kila siku mama.Nikichelewa kutoka kazini basi hupika yeye. Hivi juzi nilipelekwa kizuizini, nyumba akaihudumia yeye. Basi si mambo ya kila siku hayo. Kuna ubaya gani mama Mwengo kuitumikia aila yake?

MAMA: Aaa! Aaa! Aaa! Usiseme hivyo mwanangu! Si umefunzwa kuwa mke daima awe chini ya mume? Lazima umti na umhudumia mumeo
Si umefunzwa hayo Lanina?
Si tumefunzwa hayo tangu utotoni (uk. 41)

Katika jamii ya wanaozungumziwa katika *Kilio Cha Haki* Utamaduni umemkandamiza mwanamke na kumfanya aikubali dhuluma hii na kuiona kama jambo la kawaida.Mamake Lanina anachukulia kuwa utamaduni unamfunza mwanamke kunyenyekea kila wakati na hivyo ni sehemu ya maisha yao.Mwanamke lazima awe chini ya mwanamume jambo analolipinga Lanina.

Mwanamke aliyeelimika anazijua haki zake. Wollstonecraft (1792) anaeleza kuwa mielekeo hasi kumhusu mwanamke imesababiswa na elimu mbovu wanayopewa wanawake na wanume.

Simon De Beauvoir anazishambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha mwanamke.Asasi hizi ni pamoja na ndoa, dini na utamaduni.Anasema kwamba utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge.Mwanamke anapoolewa na kukubali utamaduni anaishia kuwa kama chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo hasi.

### 2.1.5 Mwanamke kama binadamu anayestahili kuadhibiwa

Mwanamke anachukuliwa kama binadamu anayestahili kuadhibiwa kwa hasa pale anapokosa kushirikiana na wanaume. Kachero wa kwanza anambinya Lanina kwa nguvu mabegani akitumia vidole. Lanina analia kwa maumivu. Anampiga kofi na kumvuruta masikio kwa nguvu na kumwachilia moshi wa sigara juu ya kichwa chake. Anampiga kofi na kujaribu kumwua kwa kumshika koo na kumwiita malaya. Askari anapomtia Lanina na Tereki pingu, Lanina anajaribu kujitetea lakini askari wa kwanza anampiga kofi na kumwita mpumbavu. Askari anasema:

ASKARI: (*Anampiga Lanina kofi*) wacha upuuzi wako huo! Haki! Haki! Unapigania kitu ambacho hata ukipewa hujui ukifanyie nini! Mpumbavu wee! (uk. wa 14)

*(Kachero wa kwanza anatia vidole vyake kwenye mabega ya Lanina na kumbinya kwa nguvu sana. Lanina analia kwa maumivu huku anajaribu kujikupua. Kachero anamwachilia),* (Uk. wa 22).

KACHERO WA 2: Mwenzangu Bwana Hatila ni mtu wa hasira sana. Ni afadhali kusikiliza wasia wake ufanye lile alitakalo (*Kimya)*

Naam.... Sasa turudie tena swali letu.

Ni nini hasa madhumuni yako katika kuchochea migomo hii?

*(Kimya, Lanina anashtukia kofi linalotokea nyuma linalokaribiana kumwangusha)(Uk 22-23)*

Baada ya haya yote, Lanina hakufa moyo. Aliendelea kuushikilia msimamo wake wa kupigana na udhalimu wa Bwana Delamon kwafanya watumwa katika nchi yao. Alikataa katakata kutowasaliti wenzake kama alivyofanya Tereki.

Mwanamke anapigwa kwa sababu ya ubaguzi wa jinsia. Carr (1975) anaelezea kuwa katika mataifa mengi wanawake wanabaguliwa katika kazi na hata kutoruhusiwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, lakini juhudi zinazofanywa na vyama vya miungano ya wafanyikazi kufutilia mbali ubaguzi huo.

Kathleen. N. Katika *The Sisterhood of Man,* anaeleza kuwa kulingana na sheria za Kiislamu, mwanamume ana haki ya kumpiga mke wake ikiwa hatamtii.Hata hivyo sharia inafafanua kuwa kiboko atakachotumia mume kisiwe kikubwa kuliko kidole gumba.

### 2.1.6 Mwanamke kama kiumbe asiye na haki ya kujihusisha na siasa

Mwanamke katika *Kilio Cha Haki* amedhulumiwa hivi kwamba japokuwa anashiriki katika siasa ananyimwa uhuru wa kujihusisha kikamilifu na siasa na kutoa maoni yake.

Zari anamdharau Lanina ambaye ni kiongozi wa wafanyikazi pale ambapo anasababisha mgomo. Delamon anapohofia sauti za wafanyakazi, Zari anamjibu kwa lugha ya kubeza mwanamke.

ZARI: Yaani .......Yaani ni wale....wale viongozi wao tu. Ni yule Lanina tu .....yule mwanamke mshenzi....yule.....

Delamon naye anashangaa kuwa mzozo wote wa mgomo ulichochewa na mwanamke mmoja tu na kwamba Zari na Shindo walikuwa wameshindwa kumnyoosha. Siasa za Lanina zinachukuliwa na Delamon kama za kumvunjia biashara na hivyo kukosewa heshima. Anasema :

DELAMON: (*Akipiga ngumi meza)* Lanina! Lanina tena!

*(Anasimama na kuanza kuzunguka ofisini).*

Huyu mwanamke ni punda, hana fadhila hana shukrani. Hayawani. Nimempa kazi naye amekataa. Ameniita mwizi, ati namhadaa . Ni dhamira yake, mwanamke huyu. Kunivunjia biashara yangu na kunimalizia maisha yangu. Basi atanitambua!

....leo atanitambua (uk. 66)

Delamon anamwona Lanina kama mwanamke asiye na shukrani; anayepewa kazi na kukataa. Kwake, Lanina alikuwa mwanamke wa kumvunjia biashara yake na kummalizia maisha.

Askari wa kwanza anapowatia pingu Lanina na Tereki, Lanina anajaribu kueleza azma yao lakini askari anamdharau na kumwambia kuwa alipigania kitu asichokijua. Yaani

mwanamke hajui chochote kuhusiana na siasa na akijihusisha basi na siasa za wanaume anakuwa kama malaya. Haya yanadhihirika zaidi kupitia matamshi yake.

ASKARI: Wacha upuuzi wako huo!

Haki! Haki! Utapigania kitu ambacho hata ukipewa hujui ukifanye nini!

Mpumbavu wee!

Vyombo vya usalama pia haviachwi nyuma katika kumdhulumu mwanamke aliyejiingiza katika siasa na kumchukulia kama ambaye nafasi yake ni nyumbani. Hili linadhirishwa na sanaa ya lugha ya kachero anayemwona Lanina kama mwanamke asiyekijua anachokipigania.

Licha ya dhuluma hizi, Lanina anashikilia kutowasaliti wenzake na kupinga juhudi zote za wanaume waliojaribu kumhonga kwa kumjaza fikra za ubinafsi. Kutokana na wakili tunapata kuwa utamaduni unamtukuza mwanamume huku ukimtweza mwanamke.

Wakili anamwambia Lanina kuwa ingefaa kama angejiepusha na siasa mbaya akae nyumbani kumtazama mumewe na watoto wake. Hata hivyo Lanina anaikabili hali hii ya kumkandamiza mwanamke na kumwambia wakili kuwa ingawa siasa ni mchezo mchafu basi ilibidi usafishwe. Kulingana na Lanina ulimi uliotumiwa akatiwa gerezani kwa mashtaka ya kuua ungetumiwa sawa kusafisha siasa mbaya. Wakili anasema :

WAKILI : Unajua Lanina, ingekuwa bora kwako kama ungejiepusha na mambo haya ukakaa nyumbani kumtazama mumeo na watoto wako. Siasa ni mchezo mchafu na ungewaachia waume mchezo huo.

Utangamano wa Lanina na wafanyikazi wenzake pamoja na wanaharakati wa kutetea haki za wafanyikazi unamzushia shutuma kutoka kwa wazazi na mumewe. Mwengo anamwambia Lanina kuwa hakumfahamu tena kutokana na tabia zake zilizozidi kubadilika kila wakati. Kwa Mwengo Lanina alikuwa kama mgeni. Yaani asiyejali jadi ukoo, mume na auladi. Alikuwa kama amiri wa mabadiliko. Yaani asiyekiri mila wala kujali miko. Alikuwa kama msafiri kumaanisha kwake ni kule alikokuwa.

Hata hivyo Lanina anatetea hali hii kwa kumzindua Mwengo ili atambue hali iliyowakabili wafanyikazi na kumweleza kuwa ilifaa wapiganie haki zao na wawe na msimamo thabiti. Hali kadhalika anamwambia Mwengo asiutilie mzizi utamaduni kwa kuupa uhai wala kuufuata unapowatumbukiza matatani (uk 32).

Mwengo anamchukulia Lanina kama mwanamke asiye mwaminifu kwake kwa kujihusisha na siasa za wanaume. Anamwambia Lanina kuwa kwa wiki zote alizokuwa gerezani alimweka wasiwasi na ni kama kwamba hakumfikiria – hakufahamu hisia zake. Anamwambia Lanina kuwa anaona ugumu kuishi naye kutokana na minong’ono ya watu (uk 29).

Haya yanadhihirika kutokana na maongezi kati ya Lanina na Mwengo.

MWENGO: Nipoe! Mimi nipoe! Wewe mwanamke una kichaa wewe! Umeniweka wiki zote hizi na wasiwasi halafu....halafu....unaniambia nipoe. Unafikiri mimi jiwe wewe. Sina hisia...Lanina sikiliza nikwambie. Hii ni mara ya pili sasa unatiwa nguvuni na polisi, kwa sababu zisizofahamika. Ndiyo....sababu zisizofahamika. Mimi siwezi tena kustahamili mambo haya. Naona huna haja ya mume wala watoto wewe. Lakini je sisi Lannai. Mimi mumeo, na watoto wako ? Huoni ya kwamba unatutupa kwa sababu ya msimamo wako. Nimekuwa kama....kama...ah!...kama si mume wako tena (uk wa 3)

Kutokana na maoni yetu, ni dhahiri kuwa Mwengo anamshuku mke wake Lanina kwa kutokuwa mwaminifu.

Licha ya haya, Lanina anatetea nafsi yake, anamwelekeza Mwengo kutambua umuhimu wa kustahamili. Lanina anamwambia ajaribu kumwelewa zaidi kwani iliwabidi wakabiliane na mapambano dhidi ya kazi za sulubu kama wanfanyikazi na kuwa waelewane na wasaidiane ili waweze kuzishinda tofauti za kinyumbani (uk. 35).

Babake Lanina anamwona kama mtoto aliyekengeuka kutokana na siasa zake. Anashangazwa na jinsi vijana wa kike (Lanina) wanavyotaka kuwa wazungu na wanaume huku wakitupilia mbali mila zao. Anakataa kabisa kuhusishwa na Lanina na kumkataza asimwite baba.

BABA: Baba? Umesema nini?

Babako mimi?

Mimi sikuzaa malaya! (uk. 37)

Vile vile mamake Lanina ameathirika na siasa za Lanina. Anasema:

MAMA: Ah mwanangu, tulikuwa na wasiwasi wako tu……

Lanina anamkumbusha mama kufahamu kuwa alikuwa na idhini yao na mume wake ya kufanya yote yale na kuwa hakukuwa na haja ya kujitia wasiwasi. Anamwelekeza kutambua kwamba katika kazi, lazima kupatikane malalamiko iwapo kuna unyanyasaji. Anampa mfano wa jinsi babake hulalamika makaburu wanapomnunulia mahindi kwa bei ya chini. Anamfahamisha kuwa pia hizo ni dhuluma za kijijini tofauti na zao za mjini za kuwauzia makaburu nguvu zao kwa faida yao wenyewe. Anasema:

LANINA: Hasira? Lakini hasira za nini mama?

MAMA: Ah mwanangu weee! Dunia hii huisha maneno? Kila mmoja asema lake, na babaako….ameanza kuathirika sasa.

LANINA: Lakini ni maneno gani aliyoyasikia?

MAMA: Si hizo siasa zako Lanina?

LANINA: Siasa gani mama? (uk wa 40)

Kutokana na mazungumzo haya, ni wazi kuwa wazazi wa Lanina hawaungi mkono harakati zake za kupigania hali nzuri ya wanfanyikazi.

DELAMON: *(Akipiga ngumi meza)*

Lanina! Lanina tena *(anasimama na kuanzia kuzunguka ofisini).*

Huyu mwanamke ni punda, hana fadhili, hana shukrani.

Kama hayawani

Haya yanasemwa na Delamon baada ya kusikia sauti za wafanyikazi waliogoma. Tereki anapomwarifu kuwa wapo wafanyikazi ambao wameonana na Lanina anashikwa na ghadhabu na anaamua kumkashifu Lanina.

Kathleen N. Katika *The Sisterhood Of Man* anaeleza kuwa kuna maendeleo na uwakilishi wa wanawake katika siasa na maamuzi ya maswala mbalimbali. Hii ni ishara kuwa wanawake wanahusishwa vilivyo katika jamii.Anaendelea kusema kuwa kisheria wanawake ulimwenguni wamepewa majukumu ya kisiasa katika nchi chache, lakini hawapewi nafasi ya kutekeleza majukumu hayo kiukamilifu kulingana na idadi yao.

Kutokana na utafiti wetu ni wazi kuwa kujikomboa kwa mwanamke kutoka dhuluma ya mwanaume kutachukua muda mrefu sana kwa sababu twaona kuwa mwanamke licha ya kukandamizwa, hajitokezi imara na kupinga dhuluma hiyo lakini anaiunga mkono. Mfano mzuri wa mwanamke anayeunga dhuluma mkono ni mama yake Lanina. Anataka kuendelea kushikilia utamaduni hata ingawa umepitwa na wakati.

Utamaduni umempembeza mwanaume huku ukimtweza mwanamke. Baba yake Lanina anamkemea, mama ya Lanina pamoja na Lanina. Anashikilia kuwa hataki kusikia

chochote kutoka kwa Lanina na mamake. Hataki kuwasikiliza kwa kuwa anawaona hawana adabu na kuwa yeye ndiye simba na angurumapo hataki kusikia 'lakini' zao za kijinga. Haya yanabainika kutokana na mazumgumzo ya baba ya Lanina.Anasema:

> BABA: Ala! Mbona hizi 'lakini' zenu zimekita mipaka sasa. Kila kitu ' lakini' kila kitu 'lakini *(Akimnyoshea mamake kidole)* Wee! shikeni adabu zenu. Mimi ndiye simba wa nyumba hii.Ningurumapo sitaki kuzisikia 'lakini ' zenu za kijinga *(Akimgeukia Lanina)* Na wewe binti wa shetani. Mimi si wale wanaume wengine unaowachezea. Mimi si kina Mwengo.Mimi ni dume kweli kweli. Umesikia hivyo!*(kimya (Akimtazama tena mama)* Haya, jitoto lako limefika sasa.Kaa nalo ulifunze adabu na heshima. Ulifunze maana ya uke.Uukomeshe huo udume wake. Umesikia hivyo!

Baba yake Lanina anendeleza ubabedume katika famila yake. Anajigamba kuwa yeye ndiye dume kweli kweli kwa hivyo hakuna chochote cha maana anachoweza kuambiwa na mwanamke ( Uk.38)

German Greer katika The Female Eunuch, anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa inawafanya kumilikiwa na kukosa ubinafsi na uhuru.

## 2.2 Mwanamke kama kiumbe jasiri na mwenye msimamo thabiti

Mwanamke katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* ametukuzwa na kupewa taswira nzuri inayomfanya kuheshimiwa na jamii.Jamii inayozungumziwa katika *Kilio Cha Haki* inamtambua mwanamke kutokana na uwezo wake wa kuikomboa jamii.

Mwanamke katika *Kilio Cha Haki* anajitokeza kuwa kiumbe jasiri na asiyetingishwa na lolote.Ujasiri huu unadhihirika kupitia kwa mhusika Lanina. Haya yanadhihirika Lanina anapoitwa na Bwana Delamon afisini kwake. Lanina anakataa chai na kumwambia awaeleze alilowaitia kisha waondoke. Delamon anaposisitiza waletewe chai ili mazungumzo yao yawe mazuri zaidi Lanina anamjibu bila woga :

DELAMON: Nadhani mazungumzo yetu yatakuwa mazuri zaidi, yatakuwa ya kirafiki zaidi, tukinywa chai pamoja. Tafadhali msinivunje

LANINA: *(Kwa uthabiti)*

Hatutaki chai Bwana Delamon!

LANINA: *(Anamkatiza mwenziwe)*

Kwanza kabisa malalamiko mmeshaletewa, kwa hivyo sioni kwa nini tuyakariri tena hapa. Pili sisi sio wawakilishi wa wafanya kazi wa shamba hili. Mjadala wowote juu ya malalamiko yetu ni lazima ufanywe na watu tuliowakilisha.

LANINA: *(Akimtazama tereki kwa hasira)*

Wacha kutilia nguvu uongo wao Tereki!

*(Anawageukia Delamon, Zari na Shindo)* La! Bwana Delamon

nyinyi hamkuja hapa kwa manufaa yetu. Hamkuja hapa kwa maendeleo ya nchi yetu. Mmekuja kwa maslahi na faida yenu wenyewe. Mmekuja kutudhulumu tu.

Kutumia ardhi yetu

Kutunyang'anya ardhi yetu

Kuinyonya nchi yetu

Kwa gharama ndogo isiyokuwa na thamani

Lanina anatiwa kizuizini mara nyingi lakini anavumilia. Hata anaposhtakiwa kwa mauaji ya Shindo Tereki na Delamon, ana imani kuwa atarudi na anasema:

LANINA: ...Mpenzi mama nitarudi nyumbani, nitarudi hata kama ni kifoni,.

Hata kama maiti yangu imekatika vipande elfu, elfu kumi, nitarudi nyumbani. Kama shetani nitapenya na kuziruka

Kuta hizi za matofali, nitarudi mpenzi mama hata mwangu kifoni.

Ujasiri wa Lanina unaweza kufananishwa na unaozungumziwa na Bryden M (1998) Katika *Somalia: Between Peace and War Somalia Women on the Eve of the 21$^{st}$ Centuary.* Kulikuwa na mahojiano ya mwanamke aliyesingiziwa wizi katika benki moja Somalia. Baada ya kupewa msamaha alijiunga na kikosi cha kupigana. Mume wake aliuawa vitani. Hakufa moyo aliendelea kupigana na hata kuwapelekea askari silaha usiku kisiri. Kutokana na maelezo haya mwanamke anafaa kuwa jasiri ili kukabili matatizo yanayomkumba. Kulingana na maoni yetu tunamwona Lanina kama mwanamke aliyejitolea kuwatetea wafanyakazi wenzake na jamii ili maisha yao yawe bora.

### 2.2.1 Nafasi ya mwanamke katika jamii

Mwanamke katika *Kilio Cha Haki* amepewa jukumu kuu katika jamii. Jukumu la kuzaa na kuwalea watoto linadhaminiwa sana miongoni mwa jamii za Kiafrika. Mama yake Lanina anamlea Lanina na hata kumfunza mila na tamaduni zao.

Lanina anapotoka kizuizini Mwengo analalamika kwa sababu anachelewa kufika nyumbani baada ya kazi. Kuchelewa huku kumesababishwa na msimamo wa Lanina kutetea haki za wafanyikazi. Anamwona Lanina kama asiyemjali tena, yeye pamoja na watoto anamwona kama aliyezitupa mila na kusahau wajibu wake kama mke. Mwengo ana hamaki za kibinasi ilhali Lanina ana hamaki za kuondoa udhalimu wa kibeberu. Anamdhulumu Lanina kwa kuwa ni mwanamke huku akichukulia nafasi yake kuwa jikoni. Hebu tutazame mazungumzo yao:

MWENGO: Lanina! Lanina!

Wewe unajua siku ngapi sasa umeniweka bila ya usingizi? Unajua siku ngapi sasa watoto wanakula chakula kibichi? Wewe! Wewe.... (uk. 29)

... usinifungie mdomo namna hii mimi ni mume wako ala! Umesahau? Kwa nini hunijibu! Kwa nini unanipuuza namna hii? *(kwa hasira vile vile)* angalia! Angalia namna gani watoto wanavyotaabika.

Angalia majonzi na shida zao! Halafu ati unajiita mama yao.

Haki ya Mungu wewe.... Wewe *(Akitazama chini)* Lanina unajua. .. siku hizi nakuona unachelewa kurudi nyumbani....(uk wa 30)

Kazi za kuwalea watoto zinasisitizwa naye Friedman (1963). Anaeleza kuwa katika tamaduni nyingi umama ni hali ya kuzaa na kuwalea watoto Hii kimsingi ni kazi ya wanawake. Baada ya kujifungua ni sharti mwanamke amlee mtoto hadi awe mtu mkubwa. Kwa hivyo jukumu la kuwatunza na kuwalea wana ni la lazima kwa kila mwanamke.

### 2.2.2 Mwanamke kama kiumbe mwenye mapenzi ya dhati

Mwanamke katika *Kilio Cha Haki* amechorwa kama kiumbe mwenye mapenzi ya dhati kwa wote anaotangamana nao. Mamake Lanina kwa sababu ya mapenzi yake kwa Lanina anahuzunika anapopata habari za Lanina kutiwa kizuizini.

Wakati Lanina anapotoka kizuizini anafika kwake nyumbani na kumkuta mume wake Bwana Mwengo . Mwengo anahamaki kwa kumwona Lanina. Hataki hata kumsikiliza ili amweleze alikokuwa. Lanina hakasiriki anaongea naye kwa upole .Ingawa Lanina ametoka kizuizini bado ana mapenzi kwa mume na watoto wake na anawajulia hali wazazi wake. Alipendwa na wafanyikazi hadi wakamchagua awaongoze.Ni kutokana na upendo wake ndipo anaamua kupigania haki za wafanyikazi.Tazama mazungumzo yake na Mwengo:

LANINA: Hebu Mwengo poa kidogo kwanza tafadhali. Utawaamsha watoto poa tuweze ---------- Pole Dida mwanangu nimesharudi.

Mwengo tafadhali poa moto!Mimi siwezi kuzungumza ukiwa hali hiyo. Hasira zako hazitusaidii kitu.

MWENGO: (*Bado kwa hasira* )

Haya!Haya nimeshapoa !Haya!Sema ulilonalo!Sema basi; sema na mimi nasikiliza!Sema!(*anamgeukia Dida* ) twende tukalale mama. (uk wa 30)

### 2.2.3 Mwanamke kama mfanyikazi anayewajibika

Lanina amechorwa kama mfanyakazi mwenye bidii anayewajibika. Anawahamasisha wafanyakazi wenzake kuhusu hali bora ya kazi na kuwaongoza katika mgomo ili

kumshinikiza bwana Delamon awasikilize na kuwaongeza mshahara. Mgomo huo unafaulu. Baada ya Lanina kutiwa kizuizini kisha kufutwa na Delamon anaajiriwa kwa Mzee Ingeli kama mpishi kazi ambayo anaifanya kwa bidii ili kuilisha familia yake.

Ni kutokana na mazungumzo ya Tereki ndipo tunafahamishwa Lanina amefutwa kazi.

Tazama mazungumzo yafuatayo:

TEREKI: Lanina tumekuja kukupa pole .

LANINA: Pole? Pole ya nini Tereki.

TEREKI: Ya Kutiwa kizuizini kwa muda mrefu.

Ya kufutwa kazi. Hakika ni mambo ya kuhuzunisha Lanina.

LANINA: Mzee Ingeli anataka msaada katika kioski yake. Labda nitaanza kesho.

PELEKA: Lakini hiyo si kazi ya haja Lanina ni kudunishwa huko.Mshahara bila shaka mdogo sana, na..(uk wa 49-50).

Hata baada ya Tereki kujaribu kuidunisha kazi hiyo Lanina hakati tamaa.Anamwambia Tereki kuwa mshahara mdogo haumdunishi mfanyakazi bali ni hali ya kazi.

### 2.2.4 Mwanamke kama mwanamapinduzi

Mwanamapinduzi ni yeyote aliye tayari kubadilisha hali fulani katika jamii bila hofu. Lanina anajitokeza kama mwanamapinduzi pale ambapo anawahamasisha wafanyakazi wenzake kuhusu haki zao za kazi. Wanagoma ili kujikomboa na udhalimu wa Delamon.Anafanya kila juhudi hadi wafanyakazi wanagoma na kusababisha hasara kubwa kwa bwana Delamon. Anazuiliwa kwa siku nyingi na kuteswa na askari lakini anaapa kupigana.Anamwahidi mama yake kuwa atarudi nyumbani hata kama ni kifoni.

LANINA: ............Mpenzi mama nitarudi nyumbani .Nitarudi hata kama ni kifoni.Hata kama maiti yangu imekatika vipande elfu elfu kumi,nitarudi nyumbani......... nitarudi , mpenzi, mama, hata mwangu kifoni. Nitarudi........

Hali hii ya mapinduzi imezungumziwa na Ifi Amadiume katika Gender and Sex in an African Society .Anasema kwamba wanawake wa mji wa Nigeria waliwagomea watawala kwa sababu ya ushuru mkubwa uliokuwa ukitozwa bidhaa zao sokoni na kuwafanya wakose kutengeneza faida ili watajirike kama wanaume.Mawazo kama haya pia yametolewa na Hafkin (1976). Kitendo cha hawa wanawake kilikuwa ni njia moja ya kujikomboa na udhalimu waliokuwa wakitendewa.

### 2.2.5 Mwanamke kama kiumbe aliye na uwezo wa kujitetea

Wakati wafanyikazi wa shamba la bwana Delamon wanapogoma Lanina analaumiwa. Lawama hii inamwongoza Delamon kuamuru Lanina na Tereki waletwe ofisini mwake. Delamon anawauliza Lanina na Tereki wamweleza mashtaka yao. Lanina anaghairi kuzungumza. Lakini pindi tu Tereki anapoanza kuzungumza Lanina anamkataza kuzungumza na kumwambia Delamon kuwa hawana haja ya kuzungumza zaidi kwa kuwa Delamon alishaambiwa malalamiko yao. Ikiwa kuna malalamishi yoyote sharti yawasilishwe na wafanyikazi ambao wanawawakilisha. Tazama mazungumzo haya.

LANINA: *(anamkatiza mwenziwe)* kwanza kabisa, malalamiko mmeshaletewa, kwa hivyo sioni kwa nini tukueleze.

### 2.2.6 Kimalizio

Katika sura hii tumeangazia taswira hasi na vilevile taswira chanya aliyopewa mwanamke na jamii katika *Kilio Cha Haki*. Ni bayana kuwa mwanamke amedunishwa na jamii na kuonekana mnyonge,dhaifu na maskini mbele ya mume.Mwanamke amechorwa kama kiumbe asiyezingatia maadili mema pale ambapo anajibizana na wanaume na hata kutangamana nao katika njia mbalimbali.Tumemwona pia mwanamke akijitokeza kama kiumbe kinachokandamizwa na utamaduni.Kulingana na utamaduni wa jamii inayozungumziwa katika *Kilio Cha Haki*, twaona kwamba jamii hii inashikilia kuwa mahali pa mwanamke ni jikoni na kila wakati mwanamke anafaa kunyenyekea mbele ya mume.

Licha ya hayo mwanamke amechorwa pia kwa njia nzuri.Mwanamke amepewa jukumu muhimu la kuendeleza kizazi. Anafaa kuwalea, kuwatunza na kuwapikia wana wake.Mwanamke amepewa sifa ya mfanyakazi anayewajibika katika jamii pale anapoonekana kuitunza jamii yake hata kupitia kwa mapato yake madogo.Kwa kuwa mwanamke anaijali jamii kwa jumla anajiingiza katika siasa ili kuuondoa uongozi ambao umewadhulumu kwa siku nyingi. Mwishowe anaikomboa jamii kutokana na dhuluma za uongozi.

## 3.0 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA YA PANGO

*Pango (2003)* ni tamthilia inayoyamulika matatizo yanayowakumba wanajamii wa leo. Matatizo haya ni ya kisiasa kiuchumi, uongozi mbaya, mageuzi yanayoletwa na vijana, utamaduni, na tofauti iliyoko kati ya viongozi, wazee na vijana. Licha ya hayo tunakumbana pia na matatizo yanayoletwa na ufisadi miongoni mwa wanajamii unaoendelezwa na jamii ya kale inayoamini kuwa uongozi hauwezi kushikiliwa na vijana.

Pango imechukuliwa hapa kumaanisha nchi ya watu fulani, sehemu mojawapo ya nchi, mahali ambapo rasilmali ya nchi inahifadhiwa au kimbilio la wananchi. Pangoni humu mna nyuki wanaotengeneza asali tamu sana lakini asali hii hairambwi na watu wote. Inawafaidi tu watu wachache ambao wanaliongoza Pango jinsi wanavyopenda.

Siasa zinazaoendelezwa katika tamthilia ya Pango ni za ukoo. Kupitia kwa usemi wake Ngwese tunajulishwa kuwa babu yake alikuwa ,kiongozi na wakati mmoja aling'olewa mamlakani kwa sababu ya wivu. Haya yanatokana na mazumgumzo ya Ngwese anaposema:

NGWESE: Sitopoteza wakati kutupiana maneno na mwanamke. Ni hivi sikiliza, huo wivu wako…uukome! Najua umerithi, wazee wenu waliomwonea babu wivu na hili halikumzuia kuwa chifu. Ni kilele za chura tu, hazimzuii

ndovu kunywa maji, ni kelele za mlango hazimnyimi mwenye nyumba usingizi.

KATANGO : (*Kahamasika*) la!la!la! usipotoshe ukweli. Hamna aliyemlilia ngoa kabisa. Unasikia ? Hamna.Yeye alikuwa mbaazi uliokosa maua *(mtuo)* ...akasingizia jua. Watu walichokishutumu ni matendo yake. Unasikia ?

Vijana wa Pango wanapogundua ufisadi ambao umekithiri Pangoni kwa sababu ya uongozi mbaya na siasa mbaya, wanaamua kujiunga pamoja ili wawang'oe viongozi wanaorudisha uchumi chini akiwemo Ngwese. Vijana ambao ni Katango, Kikubi na Kibwana wanajaribu kila njia ili kuuondoa uongozi mbaya lakini wanakumbwa na vizuizi vingi vikiwemo vizuizi vya utamaduni.

Katango ambaye ni mwanamke aliyesoma na mwalimu anapojitokeza na kusema kuwa anataka kuwania uongozi wa Pango anapigwa vita vikali sana na Ngwese pamoja na kundi lake na hata kupingwa na mwanamke kwa jina Mbabekazi anayeshikilia kuwa wanajamii hawatamkubali kiongozi hasa mwanamke kuwaongoza.

Uchaguzi ulipokaribia Katango alionekana kuwa na wafuasi wengi wanaomwunga mkono. Siku ya uchaguzi Katango alifaulu kuwavuta watu wengi upande wake lakini watu wachache wakamsaliti na hivyo akapokonywa uongozi na Ngwese. Ngwese aliposhika uongozi alifurahi sana lakini furaha yake haikudumu kwa kuwa alitiwa, nguvuni kwa sababu ya ufisadi. Haya yanadhihirika kupitia usemi wa polisi wa II.

Polisi II: Mzee tumekuja kukuchukua. Unatuhumiwa kufuja mali ya umma ulipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma?

Baada ya Ngwese kutiwa nguvuni wananchi walishangilia na kuimba wimbo wa ushindi huku wakimwinua Katango juu.

### 3.1 Mwanamke kama mwanamapinduzi

Katango anajitokeza kama mwanamke mwanapinduzi. Anashiriki siasa kama mwanamume. Hii ni kwa sababu anatupilia mbali tamaduni za kumwona mwanamke kama kiumbe duni na kujiingiza katika siasa. Anaamua kushindana na Ngwese ambaye anatumia mbinu nyingi kumdhalilisha zikiwemo vitisho ili awachane na siasa, lakini Katango hakukata tamaa . Anaamini kwamba hata kama yeye ni mwanamke, yeye ni mwana Pango na ana haki ya kuwania uongozi. Lengo lake ni kuleta mabadiliko katika Pango. Anasema:

KATANGO: Nina haki ya kuwania uongozi kama mwana Pango yeyote yule? (uk 20)

Katango anaamua kufanya mikutano mbalimbali kwa ushirikiano wa marafikize wakiwemo Kibwana, Kikubi, Mbabekazi na Kauleni. Mkutano wao unaandaliwa hotelini kwa bwana Kauleni ambaye anaonekana kumwunga mkono Katango katika shughuli zake za kuwania uongozi. Hata anamhakikishia Katango kuwa wako pamoja katika mambo yote kuhakikisha Katango ameutwaa uongozi. Anasema:

KAULENI: Tuko pamoja (*Wote wanageuka na kumwashiria kwa vidole gumba ishara ya kukubaliana.Wale watu wawili wanasimama upande, anaingia Ngwese*)

Kupitia kampeni za Katango, aliweza kuwapata wafuasi wengi sana. Siku ya uchaguzi, aliweza kuwavuta wafuasi wengi upande wake baada ya kuwasimulia hadithi kuhusu wanyama ambao walijiunga ili watafute suluhisho la maji. Wanyama wakubwa wakiwemo ndovu, na simba walishindwa, lakini sungura kwa kutumia akili yake aliweza kuwaonyesha wanyama mahali pa kupata maji. Katango alielekea kushinda uchaguzi huo lakini kwa vile mkono mtupu haurambwi, Ngwese aliwavuta watu wengi upande wake kwa kuwahonga kwa matunda.

Juhudi hizi za wanawake kuwania uongozi zimeangaziwa na Brydon. L. na Chant. S. (1993) Katika *Women in The Third World* akinukuu Ifeka (1975) anasema hivi "Wanawake wa jamii ya Igbo waligomea watawala wa kikoloni hadharani".

Wanawake hawa waligomea wakoloni kama njia moja ya kutafuta ukombozi.Walikuwa wakitozwa ushuru mwingi kule sokoni na wakashindwa kuchuma mali ili waweze kutajirika kama wanaume.Hii ilikuwa njia moja ya kuwakandamiza wanawake ili wasiendelee kiuchumi.

Kulingana na ripoti iliyotolewa katika '*Women: A world Report(1985)* inaeleza kuwa wanawake wanashindwa kuingia katika siasa kwa sababu ya ukosefu wa elimu na ukakamavu wao. Zaidi pia wanawake hawa hawana muda wa kushughulikia siasa. Mwanamke ambaye analazimika kufanya kazi kule nyanjani, kiwandani na jikoni ana uwezo mdogo kuliko mwanamume wa kujishughulisha na siasa.

Nawal El Saadawi kama mwanafeministi alitembelea mji wa London na kuwakuta wanawake walioshiriki katika siasa. Wanawake hawa walishiriki katika siasa ili kuleta mabadiliko katika familia zao na hata nje ya familia zao.Kwa ujumla tunaona kwamba ikiwa wanawake wanaweza kuungana kupitia siasa basi wataikomboa jamii.

### 3.1.1 Mwanamke kama mtunzi wa jamii

Mwanamke amechorwa kama mtunzi wa jamii.Katika jamii ya wana Pango wanawake wamepewa jukumu muhimu la kuwalea na kuwatunza wana. Malezi mema yanadhihirika kupitia kwa mama Katango ambaye anawalea watoto wake wa kike na wa kiume bila kuwabagua. Susa na Sota wanafanya kazi bila ubaguzi,wote wanaenda kisimani kuteka maji na pia wanaenda malishoni kuchunga ng'ombe.

Baadhi ya tamaduni nyingi za Kiafrika hutenga majukumu mbalimbali ya watoto kulingana na jinsia kwa mfano miongoni mwa jamii nyingi za ufugaji, ng'ombe huchungwa na wanaume na maji hutekwa na wanawake. Lakini mama Katango anachukua mkondo tofauti kwa kuwaelekeza wanawe.

Mama Katango ni mfano bora wa akina mama wanaoyajali maisha ya wanao na wanataka wakue wakizijua kazi zote za nyumbani .Mama anawatuma Susa na Sota kwenda kuchunga wanyama bondeni.

Sakina pia anaonekana kama mtunzi mwema wa jamii pale ambapo anamkosoa mumewe kuhusu kuwanyima Sota na Susa maji. Sakina anapenda amani na anamsihi mumewe Ngwese kuishi kwa amani na majirani zake. Anasema:

SAKINA: Ndiyo lakini ulifanya makosa kuwanyima maji.

NGWESE: (*Akiashiria*) Kwanza wewe rudi,rudi huko ulikokuwa!Utanitilia ukuba siku yangu wewe.

### 3.1.2 Mwanamke kama kiumbe jasiri na mwenye msimamo thabiti

Katango anaonyesha ukakamavu wake na akiwa tayari kutetea wanajamii kutokana na dhuluma ya wanaume. Haya yanabainika wakati ambapo Ngwese anawafukuza Susa na Sota wanapoenda kisimani kuchota maji.Ngwese anaona kuwa kisima chake ni mali yake binafsi na hakifai kutumiwa na wanakijiji. Ijapokuwa Ngwese anamdharau Katango na kumwita "wewe mwanamke" Katango haonekani kutingishwa na lolote. Anaonekana yu tayari kumkabili bwana Ngwese kwa vyovyote. Haya yanabainika kutokana na mazungumzo yafuatayo:

NGWESE: *(akijisemea)* Ah! Kisirani chenyewe hiki . Babu alisema kukumbana na mwanamke asubuhi ni kisirani. Siku nzima anaichafua (*kwa Katango).* Mwanamke unasaka nini hapa?

KATANGO: Je! Unadhani ubabe wako utanitisha mimi? Mimi siyo hao watoto unaowafukuza watakapokuchota maji.

NGWESE: (*Kwa mshtuko*) Watoto gani?

KATANGO: *(Akicheka)* Watoto gani? Hata hamnazo huachi? Hivi unadhani watu hatuna macho? *(Akionyesha usoni)* Unadhani haya ni nini? Madude ya

kukamilisha urembo wa uso? Unadhani hayaoni haya? Unasikia bwa" mkubwa? Hukuwafukuza ndugu zangu waliokuja kutafuta maji wewe; hukuwawinga kama ndege wewe?

NGWESE: Nani mwingine si wewe mwanamke hapo ulipo? *(Kwa nguvu)* naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu.

Kutokana na mazungumzo haya, tunamwona Katango akidhihirisha ujasiri wake mbele ya Ngwese. Ujasiri ambao mwanamke anafaa kuwa nao ili kupigana na dhuluma dhidi yake.

### 3.1.3 Mwanamke kama kiongozi shupavu

Katango anajitupa katika ulingo wa siasa ili kuwaokoa wana Pango. Kulingana na mila za wana Pango ni vigumu sana mwanamke kupewa uongozi kwa sababu ya mila na tamaduni zao. Wana Pango wanashikilia kuwa uongozi hauwezi kupewa mwanamke. Maoni kama haya yanatolewa pia na Ngwese na Mbabekazi. Katango anatishwa na viongozi lakini hakati tamaa. Anashikilia kuwa yeye ni mwana Pango na atapigania uongozi. Tutazame majibizano yafuatayo.

NGWESE: (*Kwa kujishasha*) Swali gani hilo? Kuna nani mwingine wa kuchaguliwa kama sio mimi? Nani niambie isipokuwa mimi ambaye ninapumua pumzi ya ukuu? Nani mwingine isipokuwa mimi ambaye nimekulia katika nyumba ya utawala?Utawala tu! *(kwa majivuno)* (Uk. 11)

KATANGO: Ndiyo maana lazima ateuliwe kiongozi afaaye!

SEKI: Na huyo kiongozi afaaye ni wewe siyo?

KATANGO: Sikusema mimi ndiye nifaaye; lakini ikiwa ni mimi kuna ubaya gani?

Kutokana na mazungumzo haya tunaona ukakamavu na ujasiri alionao Katango kutaka kuwania uongozi. Tuliyotarajia ni kwamba Seki ambaye ni babake Katango, anafaa kumwunga mkono mwanawe kwa kuonyesha ujasiri wa kuliongoza Pango. Lakini tofauti ni kwamba Seki anamdunisha Katango na kumkataza kumpinga Ngwese ambaye ni rafiki yake.

Mbabekazi licha ya kuwa mwanamke,anampinga Katango na kusema kwamba jamii haitamrusu mwanamke kuongoza Pango. Katango anamkumbusha kuwa mradi wanawake wenyewe hawajidharau,basi wanaweza kuongoza. Katango anamkumbusha Mbabekazi awachane na mambo ya zamani yaliyopitwa na wakati na waangazie mambo yaliyopo.

Kutokana na mazungumzo hayo Ngwese anajidai kuwa karibuni atakuwa kiongozi wa Pango kwa kuwa hakuna mtu mwingine ambaye ana uwezo wa kuongoza. Kwake Ngwese anaona kuwa kwa vile amekulia katika nyumba ya utawala basi hakuna yeyote atakayemzuia kuutwaa uongozi. Anazidi kumdhalilisha mwanamke kwa kusema kuwa mwanamke ana wivu mwingi sana na hivyo hawezi kuchaguliwa kiongozi. Tazama mazungumzo yafuatayo.

NGWESE: (*Kwa kujishasha)* swali gani hilo? Kuna mwingine wa kuchaguliwa kama sio mimi? Nani niambie isipokuwa mimi ambaye ninapumua pumzi ya ukuu? Nani mwingine isipokuwa mimi ambaye nimekulia katika nyumba ya utawala? Utaona tu? *(kwa majivuno).*

NGWESE: *(Akicheka)* Umesikia wapi Katango maji ya mto kuupanda mlima; niambie umesikia wapi? Mwanamke kuongoza Pango, haiwezekani kabisa! (*anatingisha kichwa*) hiyo elimu naona imekuzuzua mpaka historia ya jamii….

Ngwese anazidi kumdhihaki Katango kwa kumwambia kuwa hawezi kumtisha na lolote isipokuwa huo mdomo wake mrefu. Kwake mwanamke anaposema lolote mbele ya mwanamume ni hali ya kupayuka tu na hana lolote muhimu la kusema. Ngwese anaamini kuwa mwanamke husumbuliwa na wivu tu. Na huo wivu wa Katango ameurithi kutoka kwa wazee wake ambao pia walimwonea babu yake wivu na mwishowe akakosa kuwa chifu. Kwake Ngwese mazungumzo ya Katango ni kama kelele za chura ambazo hazimzui ndovu kunywa maji. Ndovu kwa mkutadha huu ni Ngwese na anaamini kuwa hatazuiliwa kuwa kiongozi wa Pango kwa vyovyote vile.

### 3.1.4 Mwanamke kama kiumbe msomi

Mwandishi amemtukuza mwanamke kwa kumchora kama msomi.Katango amesoma hadi akawa mwalimu. Ni kupitia elimu ndipo Katango anajua madhara ya ukeketaji wa wanawake na kukataa kukeketwa. Ni kupitia hii elimu Katango anagundua ufisadi

unaofanywa na wana Pango na kuamua kupingana na Ngwese ili apate uongozi.Usomi wa Katango unadhihirika kupitia mazungumzo yafuatayo:

NGWESE: Umesikia wapi Katango maji ya mto kuupanda mlima;niambie umesikia wapi? Mwanamke kuongoza Pango; Haiwezekani kabisa!(*Anatingisha kichwa*) Hiyo elimu ninaona imekuzuzua mpaka historia ya jamii................

Hii taasubi inaendelezwa pia na Ngoi. Ngoi anamwona Katango kama "mwanamke tu" licha ya elimu aliyonayo. Anasema kuwa mwanamke hathaminiwi na jamii na si chochote hata ikiwa amesoma .

NGOI: Ahh! Yule mwanamke mwache! *(mtuo)* Yule lazima ashajua kuwa funda la mtu mmoja halipigwi na mtu mwingine. Na hii ni zamu yako ya kuyapiga mafunda maji matamu ya uongozi! Mwache ale chaki akijua mwanamke ni nini katika jamii hii!

Ngwese anadhihirisha ubabedume anapomdharau Katango. Kuliingana na Ngwese, mwanamke awe amesoma au hajasoma ni mwanamke tu. Anaona ya kwamba mwanamke han lolote la maana la kumwambia. Haya yanatokana na mazungumzo yao anapomwambia Katango kuwa mwanamke atabakia kuwa mwanamke tu! Hata kama ameelimika. Kwake Ngwese anaendeleza taasubi ya kiume kwa kumwona mwanamke akiwa angali yule mwanamke wa enzi za mababu zetu. Ngwese haendi na wakati na hapa anatuonyesha mgongano kamili wa wimbi la ukale na usasa. Haoni kama kuna faida yoyote ya kumwelimisha mwanamke.

Baba yake Katango alimweelimisha hadi akawa mwalimu. Kulingana na maoni yetu ni kinaya kuwa licha ya elimu aliyonayo Katango baba yake haithamini hata kidogo anamwona kwamba yeye ni mwanamke kama mwanamke mwingine yeyote. Anapoingia na kumpata Katango ameshika uta na mshale anaghadhabika sana na hata kusema Katango ameenda kinyume na mila zao. Haya yanadhihirika kutokana na mazungumzo yafuatayo.

SEKI: Hudhani? Hudhani? Kwani kuna cha kudhani hapa? *(akimwangalia Katango)* Huyu utamwamini? Mwone anavyokwenda kinyume na utamaduni kabisa?

KATANGO: *(Mshangao)* utamaduni? Utamaduni gani huo?

SEKI: Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (*Kwa nguvu zaidi*) Eh! Niambie hiyo elimu ya kizungu ndiyo iliyokupa ujasiri wa kupuuza mila?

SEKI: (*Kwa sauit ya juu)* Akitikisa kichwa chake.

Kumbe ni kweli walivyosema wazee upumbavu wa mjinga ndiyo busara yake. Utawezaje kufanya jambo ambalo hawafanyi wanawake? (*Katango anataka kuongea lakini anaashiriwa asifanye hivyo)* la...usinikate kauli. Kitendo kama hicho kinaweza hata kutuletea nuhusi

NGWESE: Nani mwingine si wewe mwanamke hapo ulipo? (*Kwa nguvu*) naona babako ameshidwa nawe, labda anaistahi elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu!

KATANGO: *(Akicheka)* ati nini?

Kutokana na maoni yetu ni wazi kuwa Ngwese anaamini kiongozi sharti awe mwanamume. Vilevile historia ya Pango haina uongozi wa mwanamke. Ngwese anawakilisha wanaume katika jamii walio na taasubi kali za kiume. Ingawa Katango ni mwanamke ambaye amesoma na ni mwalimu, elimu aliyoipata haiwezi kumfanya akawa kiongozi katika Pango kwa sababu ya mtazamo hasi wa wanajamii.

Kwa maoni yetu mwanamke anastahili kupewa elimu itakayomwongoza maishani kujua haki na kujikwamua kutoka kwa dhuluma anazotendewa na mwanamume.

Kathleen N. (1979) katika *The Sisterhood of Man,* Anaeleza kuwa jamii ambayo haiwaruhusu wanawake kutangamana na maeneo mengine kando na mahali wanapoishi haioni umuhimu wa kumsomesha msichana.Anatoa mfano wa nchi ya Volta ambayo ina shirika linalotetea usawa wa wanawake.Jukumu la shirika hili ni kuwafunza wanawake usafi, ukunga, kusoma na kuandika. Licha ya hayo shirika hili pia huwafunza wanawake jinsi ya kuweka akiba.

### 3.1.5 Mwanamke kama mkombozi wa jamii.

Mwanamke amechorwa kama mkombozi wa jamii. Katango anajiingiza katika siasa na kupingana na Ngwese ili kubadilisha uongozi katika Pango.Ijapokuwa Ngwese anamshinda Katango kwa njia ya ufisadi,hakati tamaa. Anafanya upelelezi hadi anawashika viongozi fisadi waliokuwa wakiharibu rasilmali ya jamii.Mwishowe uongozi unakabidhiwa viongozi vijana akiwemo Katango.Haya yanabainika kutokana na mazungumzo yafuatayo:

KATANGO: Niliwaambia

KIBWANA: Kumbe!

KATANGO: Pango linachezewa

KATANGO: (*Akiwageukia wengine*) tuliyemwamini !

KUNDI ZIMA: Katango oyee! Katango oyee! Katango oyee! Katango anasongea katikati na kuanza kuongea.

Mazungumzo haya yanatokea pale Pangoni. Katango alishirikiana na watu wengine ili kuwatambua wezi wa Pango. Baada ya muda mfupi Mbabekazi aliingia akiandamana na polisi ambao walimshika Ngwese kwa sababu ya ufisadi.

### 3.1.6 Mwanamke ni kiumbe aliye na uwezo wa kujitetea

Katika tamthilia ya *Pango* tunaona usemi wa mwanamke umemulikwa kuonyesha kuwa anaweza kujikomboa kupitia nguvu zake za kuzungumza. Twamwona Sakina mkewe Ngwese akimkosoa bwana wake kwa sababu ya kuwanyima Susa na Sota maji. Kulingana na Sakina anaona kuwa ni muhimu kuwa na ujirani mwema na watu wengine. Ngwese ananuia kuwania uongozi wa Pango na ili afanikiwe inafaa awe na ushirikiano mwema na majirani zake.Sakina anamwambia.

SAKINA: Kisimani...? (*Ngwese anamwangalia tu*) Hamna ubaya, Si maji wayatakayo tu? Ungewaruhusu!

NGWESE: (*Akimwigiza)* Unge-wa-ru-hu-su! Hii ardhi ya nani hii?

SAKINA: Kwani wanaichukua ardhi si ni maji tu!

NGWESE: ...Mali yangu sio ng'ombe wa kijiji kukamuliwa na kila mtu,unasikia?

SAKINA: Ndiyo lakini ulifanya kosa kuwanyima maji. Watu huishi kwa undugu.

Haya mazungumzo yanatuashiria ubinafsi alionao Ngwese. Analizungushia shamba lake seng'enge ili mtu asikanyage ardhi yake. Katango pia anaonekana kuwaokoa wana Pango kupitia kuzungumza kwake. Yeye ni mwanamke mkakamavu anayeelewa haki zake. Anapinga mila zilizopitwa na wakati na uongozi mbaya unaoendeshwa na Ngwese. Yu tayari kuwakabili wanaume kwa kuwaeleza ukweli. Anajibizana na Ngwese bila uoga wowote na kumwonyesha kuwa yeye si mwanamke tu bali mwana Pango aliye na uwezo wa kuongoza Pango. Anasema :

KATANGO: (*Akicheka*) Ati nini?

NGWESE: Hanitishi mwanamke kamwe!(*Mtuo) Karibuni* utakoma, utanywea Kabisa! Najua karibuni itakuwa fursa yangu ya kuwa mlinzi wa Pango.

KATANGO: (*Akicheka*) Utakuwa nini unasema?

NGWESE: Mlinzi wa Pango!

KATANGO: Atakuchagua nani? (Uk 10-11)

Haya mazungumzo yanabainisha ukakamavu alionao Katango, amekataa kudhalilishwa na mwanamume. Tamaduni nyingi za Kiafrika zinamnyanyasa mwanamke kiasi cha kwamba hawezi kuzungumza mbele ya mwanamume, lakini tunamwona Katango akikaidi haya yote kuokoa jamii.

### 3.1.7 Mwanamke kama kiumbe anayepinga mila zilizopitwa na wakati

Katango anamwambia baba yake Seki kuwa kushika mata na mshale hakuna ubaya wowote. Baba anashikilia kuwa mwanamke hafai kushika mata na mshale kwa kuwa mtu anaweza kupatwa na nukusi. Lakini Katango anayapuuzilia mbali kwa kusema kuwa huo ni ushirikina. Kulingana na mila, ilikiwa wazi kwamba kila mwanamke apashwe tohara. Iliaminika kuwa kitendo hiki kilipunguza hisia za mapenzi miongoni mwa wanawake. Kwa kuwa Katango amesoma na kujua ubaya wa tohara, anagoma kutahirishwa.Tendo hili linamghadhabisha Seki na analitaja wakati wanapozungumza na Katango na kusema :

NGWESE : Ushirikina gani? (*kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu;uboho wa mifupa ya jamii ndio unauita ushrirkina? Wewe tangu ugomee kupashwa...

Simon De Beauvoir (1949) katika *The Second Sex* anasema kuwa mwanamke anapoolewa hufungwa katika pingu za utamaduni zinazomfanya kukubali kudhalilishwa. Mwanamke anapokubali tamaduni hizo hutumiwa kama chombo cha kuendeleza tamaduni hizo zalilishi.

### 3.1.8 Mwanamke kama kiumbe aliye na uwezo wa kuwaunganisha wenzake

Mbabekazi alipinga uongozi wa Katango kwa sababu ya mila na tamaduni zao. Aliweza hata kuhongwa na Ngwese na akawavuta wafuasi wengi wa Katango wakarudi upande wa Ngwese. Lakini baada ya kugundua udhaifu uliokuwa miongoni mwa wanawake, akishirikiana na Katango wanafanya upelelezi kisha kugundua maovu yaliyokuwa

yakifanywa Pangoni. Katango anawakusanya wanawake kisha kushtaki ufisadi uliokuwa ukifanywa na Ngwese, Seki na viongozi wengine.Mbabekazi anapowasili na polisi kule Pangoni anamkuta Katango na akina mama wengine wamewashika Seki na Ngwese wakishiriki ufisadi.Askari anawashika Seki, Ngwese na viongozi wengine. Kitendo hiki kinatamatisha ufisadi nchini Pango na jamii inaokolewa kupitia kwa vijana kama Katango, Mbabekazi, Kibwana na Kikubi. Katango anainuliwa juu ishara ya ushindi na ukombozi katika nchi ya Pango. Tazama yafuatayo :

*(Wakati huu anaingia Mbabekazi amefuatana na polisi wawili. Watu wanatazamana, kimya)*

NGWESE: *(Kafurahi)* Ahh! Kumbe mmefika ehh.

POLISI: Tumefika ndiyo!

NGWESE: Basi mnaona,mnaona ninavyotatizwa na hawa? Siwezi hata kufanya kazi yangu ipasavyo!

POLISI: Hawezi ehhh?

NGWESE: Siwezi kabisa!

*(Polisi wa pili anamsongea)*

POLISI WA 2: Mzee, tumekuja kukuchukua.Unatuhumiwa kufuja mali ya umma ulipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma!

### 3.1.9 Mwanamke kama Kiumbe anayewajibika

Wanawake wengi sana wanaonekana kuwajibika katika tamthilia ya *Pango*. kwanza kabisa tunamwona Katango akionyesha uwajibikaiji wa hali ya juu katika jamii. Anagundua ufisadi unaoendeshwa na viongozi wa Pango na anaamua kuwania uongozi

ili aiokoe jamii kutokana na kunyanyaswa na viongozi. Juhudi zake zinazaa matunda pale ambapo anashirikiana na wanajamii wengine kuwachunguza watu wanaochezea Pangoni. Wanajamii wanashtuka kugundua kuwa viongozi wao wenyewe waliowachagua ndio wanaofaidika kutokana na asali ya wana Pango. Mwishowe wafisadi wote wanatiwa mbaroni.

Katango pia anawahamasisha wanawake kuhusu haki zao kupitia kwa kusema na kuasi mila na desturi, anawaunganisha pamoja kupigana na udhalimu wa wanaume. Mamake Katango anawajibika pale ambapo anawafunza wanawe wa kike na wa kiume kazi za nyumbani kama kuteka maji na kupeleka ngombe malishoni. Anawaeleza umuhimu wa Pango na hivyo hawapaswi kucheza Pangoni. Mama anahakikisha kuwa wanawe na mume wake wamepata chakula, ingawa mume wake hawajibiki kwa lolote, mama anaendelea kufanya kazi za nyumbani zikiwemo kuchunga watoto, kutafuta kuni, kupembua nafaka na kupika. Anamwunga mwanawe Katango mkono inapogunduliwa kuwa Seki ni miongoni mwa wanaocheza Pangoni.

Mbabekazi anawajibika pale ambapo anawaongoza polisi kuwashika wafisadi Pangoni. Mkewe Ngwese, Sakina anawajibika pale ambapo anachukua jukumu la kumkosoa mume wake kwa kosa la kuwanyima Susa na Sota maji na kisha kukizungusha kisima seng'enge ili shamba lake lisikanyagwe na yeyote.

### 3.1.10 Mwanamke kama kiumbe aliyeelimika

Katango ni mwanamke ambaye amesoma hadi akahitimu kuwa mwalimu.Ni kupitia elimu hii ndipo anazitambua haki zake kama mwanamke na kama mwana Pango, ambaye yuko tayari kupigana na wanaume walio na uongozi mbaya. Katango anagundua kuwa viongozi katika nchi ya Pango akiwemo bwana Ngwese wanatumia mamlaka yao vibaya kwa kufuja mali ya wananchi. Anaamua kumpinga bwana Ngwese wakati wa uchaguzi. Ni kupitia elimu ambapo Katango anatambua baadhi ya mila zimepitwa na wakati kama tohara kwa wanawake, kutoshika mata na mshale na mwanamke kutothaminiwa na jamii. Katango anasisitiza kuwa mwanamke ni mwana *Pango* kwa hivyo ikiwa atapewa uongozi ataongoza. Anasema *(Kwa mshangao)*: Mwanamke ana nini, si ni mwana Pango pia? Si anaweza kuongoza? Mwanamke nguzo... (*mtuo*) Kuongoza tu; Kutamshinda mwanamke kuongoza tu!

### 3.1.1 Mwanamke kama mzalendo

Mzalendo ni mtu ambaye anaipenda nchi yake na yuko tayari kuitetea kwa hali zote.Kwa sababu ya upendo wake Katango anaamua kupigania uongozi katika Pango. Aligundua ufisadi uliokuwa ukifanywa Pangoni na kuamua kuukomesha kupitia njia ya kuwabwaga viongozi.Anakataa kudunishwa na vitisho vya Ngwese na hata anaposhindwa na Ngwese anafanya upelelezi hadi wezi wa Pango wanashikwa.Anasema:

KATANGO: Ubinafsi umemleavya kabisa uchoyo umevotana na pumzi yake hiana inatoka katika kinywa chake...... Damu iliyomwagika na makafara wa ukombozi haikuwa sadaka ya kutosha?Haikuwa msingi wa undugu?

Haikuwa gundi la ujamaa wetu? Mbona? Mbona tunaisaliti kafara yao? tunaisaliti imani yao? Tunaisaliti ndoto ya waliotutangulia? (uk wa 9)

Kutakana na usemi huu Katango anataka jamii iwatambue na kuwaheshimu walioikomboa nchi yao.

### 3.2 Mwanamke kama kiumbe asiye na haki ya kuwania uongozi

Katika tamthilia ya Pango mwanamke licha ya kuchorwa akiwa na taswira chanya amedunishwa na jamii na kuonekana kama kiumbe dhaifu, mnyonge na asiyeheshimika. Mwanamke anachukuliwa kama asiye na haki ya kuwania uongozi kwa sababu jamii haimheshimu. Siasa zinachukuliwa kama ni za wanaume pekee.Katango anapoonyesha juhudi za kuwania uongozi anakumbwa na pingamizi nyingi. Pingamizi hizi zinatoka kwa wanaume na hata wanawake.Babake Katango anamkanya mwanawe dhidi ya kushiriki katika siasa kwa kusema kuwa ni kinyume cha utamaduni. Mbabekazi ambaye ni mwanamke kama Katango anampinga Katango kwa kusema kuwa utamaduni hautamruhusu mwanamke kutawala kwa kuwa unamdharau.Tazama mazungumzo yafuatayo:

SEKI: Si kweli eehh!!Basi niambie pia si kweli unanuia kumpinga kwenye uongozi wa Pango?Sema pia huo si ukweli?(*Mama anageuka kumwangalia binti yake kwa mshangao)*

MBABEKAZI: Ndiyo lakini ........... jamii inawadharau wanawake. ( uk 27)

Juhudi za wanawake kuwania uongozi zimeangaziwa na Brydon L. (1963) katika Women in The Third World. Anasema wakati mmoja wanawake wa Igbo waligomea watawala wa kikoloni

hadharani kwa sababu ya ushuru mkubwa waliokuwa wakitozwa sokoni.

### 3.2.1 Mwanamke kama kiumbe dhalili

Katika tamthilia ya *Pango* Onyesho la tatu linapoanza,mama anashughulika kupembua pembua nafaka,huku akiimba. Kutokana na wimbo wa mama inabainika kuwa mume hashughuliki hata kidogo katika kazi za nyumbani. Lakini punde tu anaporudi kutoka matembezini anadai chakula. Hata baada ya kushughulika kufanya kazi hii yote, mume bado hakosi kumlaumu.Mama anawachiwa kazi za kupembua nafaka, kutafuta chakula na kuwatunza watoto huku mume wake akiwa anatoka nyumbani bila kusema anakoenda.

Vitendo vya kuwawachia wanawake kazi nyingi na za hadhi ya chini wazitekeleze vinajitokeza katika tamthilia ya *Pango.* Mamake Katango anashughulika na kazi za nyumbani kwa kuhakikisha kuwa amewatafutia wanawe chakula na pia kumpa mume wake chakula anapowasili nyumbani. Vilevile Katango anashindwa na Ngwese katika uchaguzi kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kuwahonga wapiga kura. Ngwese anafaulu kuwahonga wapiga kura akitumia matunda (uk 50).

Kulingana na Braydon L. na Chant (1993:58) katika *Women in The Third World* wanasema kuwa kazi ambazo zinafaa kutekelezwa na wanawake ni kama kupika kila siku, kufagia, kuosha, kutunza watoto wadogo na mara nyingi kutafuta kuni na kuteka maji. Haya ni majukumu muhimu kwa mwanamke katika tamthilia ya *Pango.*

Walitoa mfano wa mwanamke kutoka Ghana ambaye anaamka kuanzia saa kumi alfajiri. Huyu mwanamke anafanya kazi ya kupika chakula ili auze na kulisha wanawe kabla waende shuleni.Anahakikisha kuwa nyumba yake ni safi,anaenda kulima shambani, baadaye anarudi kuwatayarishia wana kishuka na jioni anawaandalia chajio. Licha ya hizi shughuli zote anafaa kuuza chakula chake sokoni kabla ya kurudi nyumbani usiku.

Croll (1981) anaeleza kuwa ingawa wanawake waliahidiwa msaada kutoka kwa nchi zao ili kupunguza kazi zao za nyumbani, lakini wanawake bado wanafanyishwa kazi maradufu huku wakilipwa mishahara duni.

Maelezo mengine yanatokana na ripoti iliyotolewa katika: *A World Report (*1985*)* Inaeleza kuwa ulimwenguni kote tamaduni nyingi hushikilia kuwa kazi za nyumbani ni za wanawake. Utamaduni unamkadamiza mwanamke kwa kufanya kazi nyingi ndani na nje ya nyumba yake na hivyo kumlazimisha afanye kazi maradufu.

Kutoka Marekani Marilyn French kama mwanaharakati wa maswala ya wanawake alitembelea India katika kijiji cha Gujerat hadi Delhi na Ahmedabad. Katika miji hii wanawake ambao wako katika tabaka la kati wanaajiri wafanyikazi kuwasaidia kufanya kazi. Lakini wanawake maskini wanafanya kazi zote za nyumbani na pia kufanya kazi za mijengo. Katika sehemu hiyo ya India, mwanamke anayefanya kazi ya kuajiriwa hupandishwa cheo kulingana na jinsi mume wake anavyojulikana. Pia mshahara wa mwanamke maskini hupewa mume wake.

### 3.2.2 Mwanamke kama kiumbe kinachokandamizwa na utamaduni

Kulingana na jamii inayozungumziwa katika *Pango* inabainika kuwa utamaduni wa kukeketwa kwa wasichana na kupigwa kwa wanawake bado unashikiliwa na jamii. Katango anatishwa sana na Ngwese kwa kumwambia kuwa atampapata makofi ili aweze kumtia adabu. Ngwese anaendelea kumwambia Katango kuwa anatakiwa kuolewa ili atiwe adabu na mume wake. Ngwese anaendeleza ubabedume dhidi ya wanawake. Anaamini kuwa sharti mwanamke apigwe kama ishara ya kumtia adabu.

Katika tamthilia ya Pango kuna ule mgongano wa wimbi la kale na la sasa. Kibwana anashikilia kuwa Katango anafaa kuwa kiongozi lakini Mbabekazi anapinga kwa kusema kuwa mila na desturi haziwezi kumruhusu mwanamke kuwa kiongozi wa Pango. Mazungumzo yafuatayo yanadhihirisha haya:

MBABEKAZI: *(Kwa sauti ya unyonge*) ndiyo ana ujasiri sikatai lakini.......(*Mtuo)* Lakini ipo haja gani kufanya jambo ambalo unajua halitafanikiwa?

KIBWANA: Mbona asifanikiwe.

MBABEKAZI: Haiwezekani! *Culture, culture* bwana unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? *We are not yet there* (uk 25).

Mazungumzo haya yanatudhihirishia waziwazi jinsi wanawake wanavyojidunisha wenyewe. Mbabekazi ni mwanamke kama Katango, badala ya kumwunga mkono mwenzake katika uongozi, anampinga kwa kusingizia *culture.* Hata hivyo, Kikubi anaonyesha imani kuu kwa Katango na anamkashifu Mbabekazi na kumwambia kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke. Mbabekazi anawakilisha wanawake ambao

wamesoma lakini bado wanashikilia utamaduni wa kumdunisha mwanamke. Kulingana na Seki anaona kuwa ni mwiko kwa Katango kugomea kitendo cha tohara kwa sababu kilikuwa kinatekelezwa kwa kila mwanamke. Seki anamwona Katango kama aliyeasi utamaduni na hivyo ameasi jamii yake.

.Katika makabila mengi ya Afrika kukeketwa kwa wasichana huwa ni tendo la kuhitimu kuingia ukomavu.Brydon L. Na Chant (1989) akinukuu Mclean (1985) ,anasema

> "Ingawa lengo la utahirishaji laweza kuwa kupunguza hamu ya mwanamke, ukweli kutokana na maoni ya utabibu ni kuwa ukeketaji wa kinembe unapunguza uitikaji lakini haundoi haja ambayo ni mahitaji ya kisaikolojia".

Mbali na maelezo ya wataalam hawa, ukeketaji humletea mwanamke matatizo mengi yakiwemo shida wakati wa uzazi,uvujaji wa damu,utoaji wa mkojo kiholela,kuwa na maambukizo ya magonjwa mbalimbali.

Vilevile katika tamthilia ya *Pango,*Katango anabaguliwa na babake mzazi.Anaona kwamba mwanawe anampinga rafiki yake Ngwese na hafai kuwania uongozi.

SEKI: Si kweli eeh! Basi niambie si kweli unanuia kumpinga kwenye uongozi wa Pango? Sema huo pia si kweli?

KATANGO: Nina haki ya kuwania uongozi kama mwana Pango yeyote yule?

SEKI: (*Kwa sauti ya juu*) Unajua kichwa cha nyoka hakistahimili kilemba wewe?

> Ndio huo usasa wenu umekupa kiburi cha kuinua kichwa na kukigotesha jabalini chini kama mjusi? Hujasikia kuwa kuna majabali yaliyokwewa na mjusi?

Huu usemi unadhihirisha kuwa Katango hafai kuwania uongozi hata kidogo.Yeye amefananishwa na mjusi ambaye hawezi kukwea jabali.

Brydon, na Chant S. (1989:50) Katika *Women in The Third World* wanaeleza kuwa "Katika jamii nyingi za ulimwengu,uvishwaji wa ufalme ulitegemea babake mtu huyo, hivyo mali ilirithishwa na asili kufuatwa kutegemea kizazi cha mume"(TY)

Kutokana na maelezo haya tunaona kuwa kulikuwa na ubaguzi uliowaathiri haswa wanawake katika tamaduni za waafrika na hivyo basi Katango ni miongoni mwa hao wanawake.Kwa vile ukoo wa Katango haukuwa miongoni mwa koo tawala basi Katango hangepata uongozi.

Ngwese anamwona Katango kama mwanamke asiye na adabu. Ngwese anaendeleza ubabedume kwa kujiona kuwa yeye ni mume na yu huru kumpiga Katango makofi. Anaona kwamba Katango amekosa adabu na ili awe na adabu ni shati aolewe ili mume wake amtie adabu. Hapo bwana Ngwese anajaribu kutuonyesha kuwa mwanamume peke yake ndiye ajuaye kumtia mkewe adabu. Jambo hili si la kweli kabisa kwanza tunapoangalia malezi ya watoto twaona kuwa hulelewa kwa muda mrefu na mwanamke. Ikiwa kuna watu wowote wanaojua adabu ni nini basi ni wanawake. Anasema:

NGWESE: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira*) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu!Unatakiwa kuolewa utiwe adabu na mumeo.

Hayo yanadhihirika kutokana na sauti ya huzuni aliyonayo Katango. Katango anawakilisha wanawake walio katika kizazi kipya. Hawa wanawake walikubaliana kuungana pamoja ili kuondoa uongozi mbaya nchini Pango. Walikuwa mashujaa na walikuwa tayari kujikomboa kutoka kwa dhuluma waliyokuwa nayo kwa muda mrefu. Wakaanza harakati za kujikomboa lakini walipokuwa katikati wengi wao waliachilia gogo lile na wakakimbia na kuwasaliti wenzao. Kwa hivyo ikawa vigumu kwao kujikomboa.

Kulingana na Ramazanoglu. (1989:4) *katika Feminism and Contradictions of Oppression* anaeleza kwamba wimbi mpya la Ufeministi limemulika migawanyiko mingi iliyoko kati ya wanawake ambayo inahusisha mawanda makubwa ya wanawake. Anaendelea kusema kuwa wanawake wamekandamizwa sana na wanaume na wanaishi katika jamii ambazo zinachukulia ukandamizwaji huu kama wa kawaida na wa kutamanika, lakini pia wanawake wanadhulumiana wao kwa wao .Ngwese anaamini kuwa mwanamke ni sharti achapwe na mume. Mume ndiye tu anayeweza kumpa adabu mwanamke. Alipoambiwa ukweli kuhusu babu yake alikasirika sana nusura amzabe Katango makofi.

Ngwese anasema hivi :

NGWESE: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira)*

Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu. Unatakiwa kuolewa, utiwe adabu na mumeo!

Anapoona kuwa Katango amemshinda kwa mawazo na anayoyasema ni kweli, anakasirika na kusema yafuatayo.

NGWESE: Basi nitakunyamazisha mimi! *(kwa hasira)* karibuni tutaonana!. Tutaona ni nani aotaye! (*anaondoka afikapo mlangoni anasimama na kugeuka)* kuna siku itakuchea, siku moja nakwambia. *(anapaaza sauti)* siku hiyo utajuta nakwambia! Utajuta karibuni nakwambia! Mimi ni kimbunga, subiri tu *(anaondoka)*

Mifano hii ya kupigwa kwa mwanamke inaelezwa na Elam Y. (1973) katika *The Social Roles of Hima Women in Uganda* ambapo anaeleza kwamba mwanamke alistahili kupigwa pale alipokosa kutekeleza majukumu yake.

Katika tamthilia ya *Pango* Kikubi na Kibwana wana imani sana na Katango na wanamwunga mkono kwa juhudi zake za kutaka kuwa kiongozi wa Pango. Wanasema:

KIKUBI: (*Kwa hamu*) Haya basi tupe uhondo nasi tutereme (*akimhimiza)* ni *stori* gani hiyo?

KIBWANA: Ni hii ya huyu mwenzetu anayetaka kuliongoza Pango!

MBABEKAZI: Katango?

*(Kibwana anaitikia*)

KIKUBI: Ahh huyo? *(mtuo)* Nimesoma naye….

aliwahenyesha wanaume ile mbaya kutokana na misimamo yake.

Ana ujasiri sana *beibe* Yule!

MBABEKAZI: Sema alikuhenyesha wewe….!

KIKUBI: Sio mimi *aisee* ni wengine!

MBABEKAZI: *(Kwa sauti ya unyonge)* ndiyo ana ujasiri sikatai lakini….*(mtuo)*

Lakini ipo haja gani kufanya jambo ambalo unajua halitafanikiwa?

KIBWANA: Mbona asifanikiwe?

Kulingana na mazungumzo haya Kikubi na Kibwana wana matumaini makubwa sana kwa Katango kupata ushindi. Hata hivyo Mbabekazi ambaye ni mwanamke kama Katango anapinga nia ya Katango kuongoza Pango huku akisingizia kuwa watu hawatakubali mwanamke awaongoze kwa sababu ya *culture*. (uk 27)

Katika mazungumzo yao Kikubi anaendelea kumhimiza Katango kujitokeza ili aweze kuwa kiongozi wa Pango. Anamwuliza Katango iwapo wakati huu watautwaa uongozi wa Pango au watabakia kuwa viongozi wa kesho. Katango anamjibu kuwa watautwaa uongozi ikiwa watashirikiana. Kauleni na kikubi wako tayari kumsaidia Katango katika mipango yake ili autwae uongozi.(uk wa 27)

Baada ya Katango kupokonywa ushindi na Ngwese, babu alimtembelea nyumbani ili kumliwaza. Kulingana na babu Katango alipokonywa ushindi. Anampongeza Katango kwa ujasiri wake na kumsihi asikate tamaa. Tazama mazungumzo haya:

BABU: Eh naona, huna huzuni kama uliyokuwa nayo siku ile (*Anamwashiria asogea alipo*). Ulipokonywa ushindi kama fisi wanavyoing'wafua nyama iliyoko kinywani mwa simba. *(Anapaaza sauti*) Katango kijukuu, usife moyo, mambo hubadilika kama hujui maisha ni matembezi kwenye daraja bovu.

KATANGO: Wengine wanakata tamaa babu!

BABU: Kwa nini?

KATANGO: (*Akishusha mabega*) Hali itabaki kama zamani. Si ni heri tu kumwachia huyo Ngwese na watu wa aina yake kila kitu....hata wenzangu wananiambia kuwa sisi vijana hatuna nafasi kabisa. Kwanza wanawake nao...

BABU: *(Anamkatiza kauli huku akitikisa kidole cha mkono wa kulia*)

Babu anaendelea kumhimiza Katango asikate tamaa, awe na moyo wa subira na uvimilivu. Anampa mfano wa kuku ambaye anachukuliwa na mwewe. Mwenye kuku hawezi kumrushia mwewe mayai ya kuku kwa kuwa kuku wake amenyakuliwa. Akimrushia mwewe mayai basi atabaki bila kuku na atakuwa ameenda hasara. Babu anaendelea kumwambia Katango kuwa ubaya wa Ngwese utajulikana hivi karibuni. Kulingana na mawaidha ya babu ana uhakika kuwa wakati utawadia ambapo vijana wataongoza Pango. Babu anamweleza mama kuwa vijana ni tegemeo la jamii ya wana Pango. Ni wajibu wao kuwahimiza hata hali inapokuwa ngumu. (uk wa 59-60)

### 3.2.3 Vitisho vinavyomkabili mwanamke

Mwanamke anapogundua kuwa kuna ufisadi Pangoni anashikwa na hamu ya kuiokoa jamii kutokana na ufisadi huo. Lakini pindi tu Ngwese anapogundua anaanza kutumia vitisho ili amwogopeshe Katango. Anamtisha Katango kwa kumwambia kuwa atampapata makofi.Ngwese anamtia Katango kitata ili asizungumze.Anamtumia watu wanaomvizia na kumwonya awachane na ndoto ya kuwa kiongozi wa Pango.Tazama yafuatayo:

NGWESE: Nani mwingine si wewe mwanamke hapo ulipo?*(kwa nguvu)*Naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi hiyo elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu.

NGWESE: Basi nitakunyamazisha mimi!*(kwa hasira*) Karibuni tutaona! Tutaona ni nani aotaye! (*Anaondoka afikapo mlangoni anasimama na kugeuka*)Kuna siku itakuchea, siku moja nákwambia.(*Anapaza sauti*) Siku hiyo utajuta,utajuta nakwambia!Mimi ni kimbunga subiri tu! (*Anaondoka*)

Georgina .A. (1995) katika *Adiplomacy of the Oppressed,* anasema kwamba wanawake wengi wanaogopa kuwashtaki waliowatendea maovu kwa sababu ya vitisho kutoka kwa wanaume .Baadhi ya wanaume hao huwatisha kwa kuwaambia kuwa watauawa ikiwa vitisho hivyo vitajulikana na watu wengine.

### 3.2.4 Mwanamke kama kiumbe asiye na msimamo thabiti

Mwanamke amechorwa kama kiumbe asiye na msimamo thabiti na haya yanadhihirika kupitia kwa mhusika Mbabekazi. Mwanzoni Mbabekazi alionekana kushikilia utamaduni sana. Alimpinga Katango alipojitokeza waziwazi kuhusu kuwania uongozi katika Pango.

Anahongwa na Ngwese wakati wa uchaguzi. Mwishowe anawaleta askari kumshika Ngwese na viongozi wengine ili kumaliza ufisadi Pangoni. Haya yanabainika kutokana na mazungumzo yafuatayo:

MBABEKAZI: Haiwezekani! *culture,culture* bwana, unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe?*We are not yet there.*

KATANGO: .....Sasa macho tumeyafungua

Sasa upofu tumeupofua

Sasa vinywa tumevifungua

Maovu nayo tumeyafukua

*(Wakati huu anaingia Mbabekazi amefuatana na polisi wawili.Wanatua wanatazamana Kimya)*

### 3.2.5 Kimalizio

Katika sura hii tumeshughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia ya Pango. Mwanamke amechorwa kama kiumbe dhalili pale ambapo anaonekana kutokuwa na msimamo mmoja na mwanamume. Mwanamke anachukuliwa kama chanzo cha mikosi na visirani anapokutana na mwanamume.Hii ni kwa sababu jamii anamoishi mwanamke inamfunga katika pingu za ndoa zinazomkandamiza na kumfanya aonekane kiumbe duni. Tumemmulika mwanamke akiwa kiumbe aliyedhalilishwa na utamaduni. Utamaduni unamtarajia mwanamke anyenyekee mbele ya mume. Kulingana na maoni yetu hizi ni baadhi ya tamaduni ambazo zimepitwa na wakati na zinahitaji kurekebishwa na wanajamii. Mwanamke anabaguliwa kisiasa kuwa siasa zinamithilishwa na wanaume. Mwanamke amemulikwa kama mkombozi wa familia,kiumbe msomi , kiongozi shupavu, kiumbe jasiri, mtunzi wa jamii na mwanamapinduzi

# SURA YA NNE

## 4:0 HITIMISHO

Tumeaangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Kilio Cha Haki* (1981) na *Pango* (2003) kupitia tafiti zetu tumeweza kuona kwamba mwanamke amepewa taswira hasi na chanya katika tamthilia hizi mbili.

Katika Sura ya Pili tumeangazia taswira ya mwanamke katika *Kilio Cha Haki.* Tumeangazia njia ambazo zimemtukuza mwanamke na vilevile njia ambazo zimemdunisha.Mwanamke amemulikwa kama mfanyakazi mwenye bidii pale ambapo anaonekana kufanya kazi kwa bidii ili kuilisha jamii yake. Mwanamke amemulikwa pia kama mkombozi wa jamii pale anapowahamasisha wafanyakazi kuhusu haki zao kisha wanashiriki katika mgomo unaosababisha hasara kubwa katika shamba la bwana Delamon. Mgomo huu ulikuwa umshinikize Delamon awaongeze mshahara na kuboresha hali ya maisha ya wafanyikazi.

Mwanamke amechorwa kama kiumbe asiyekuwa na haki ya kushiriki katika siasa.Jamii inayozungumziwa ina msimamo kuwa mwanamke hafai kujihusisha na siasa kwa kuwa siasa ni mchezo mchafu na unafaa uwachiwe wanaume. Licha ya pingamizi hizi zote mwanamke anaonyesha ujasiri wa hali ya juu anapojihusisha na siasa na kuvumilia dhuluma anazofanyiwa ili aweze kuikomboa jamii. Mwanamke amekandamizwa na utamaduni kiasi cha kutokuwa na usemi mbele ya mume.Kulingana na jamii inayozungumziwa mwanamke alifaa kunyenyekea kila wakati mbele ya mume.

Mwanamke anapuuzwa na kuchukulia kama mchochezi wa jamii. Anadhalilishwa pia kupitia kazi anazozifanya.Mamake Lanina anamkumbusha Lanina kuwa ni wajibu wake kumshughulikia mume wake, kumtunza na kuwapikia watoto.Kulingana na maoni yetu jamii ya wanaozungumziwa katika *Kilio Cha Haki* inamdunisha mwanamke na kumfanya aonekane mnyonge asiyeweza kufanya kazi nyingine muhimu isipokuwa kukaa jikoni na kufanya kazi za nyumbani na asitarajie mume wake kumsaidia kazi yoyote.

Lanina anajaribu kuikomboa jamii lakini juhudi zake zinapingwa na wanajami. Askari wanampiga na hata kujaribu kumbaka lakini licha ya pingamizi zote Lanina anaapa kutowasaliti wafanyikazi. Kulingana na utafiti wetu tunaona kuwa juhudi anazofanya Lanina kuwahamasisha wafanyikazi ni mwanzo wa ukombozi wa jamii.Ikiwa Lanina angefaulu kupitia mgomo wa wafanyakazi,basi jamii ingekombolewa. Kulingana na utafiti wetu ni wazi kuwa ili jamii ikombolewe sharti kuwe na ushirikiano kati ya mwanamume na mwanamke.

Tumewaangazia pia wanaume walio tayari kuwaunga wanawake mkono.Mfano wa hawa wanaume ni Musa, Dewe, babu na Mzee Ingeli. Hawa ni baadhi ya wanaume ambao wanazitambua juhudi zinazofanywa na wanawake katika kuikomboa jamii.

Katika Sura ya Tatu tumemwangazia mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii. Mwanamke amepewa nafasi nzuri na mwandishi na anaonekana akikua kutoka kwa yule mwanamke asiyedhaminiwa hadi kuwa mkombozi wa jamii. Katango anawakilisha wanawake wakakamavu na jasiri walio tayari kuwaokoa wanajamii kutokana na

dhuluma za uongozi mbaya .Anashiriki mikutano ya siasa na hata kuwashawishi wana Pango kuwapigia kura watu waadilifu. Anakashifu ufisadi unaofanywa na Ngwese pamoja na washirika wake. Vitisho anavyopewa na bwana Ngwese na wafuasi wake havimvunji moyo hata kidogo.Anapigana na viongozi fisadi hadi anawatia ndani na kuikomboa jamii.

Vilevile waandishi wa tamthilia za *Kilio Cha Haki* na *Pango* wamemtukuza mwanamke na kumpa majukumu muhimu ayatekeleze katika jamii. Juhudi za mwanamke zimebainika wazi pale ambapo anaonekana kujihusisha na siasa.Mwishowe kupitia kwa ujasiri wake anaikomboa jamii.

Tulitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika katika utafiti wetu.Tumegundua kwamba Miongoni mwa jamii zinazozungumziwa katika *Pango* na *Kilio Cha Haki* wanawake wanadhulumiwa na wanaume. Wafeministi kutoka mataifa mbalimbali wanafanya jitihada za kutetea haki za wanawake. Kulingana na utafiti wetu ni kweli kwamba wanawake wamepiga hatua kubwa katika kutetea haki zao.Ili kupatikane ukombozi kwa wanawake wote duniani tunahitaji msaada wa wanaume katika kulishughulikia swala hili. Wanaume watakapojiunga na wanawake kupinga dhuluma dhidi yao basi jamii nzima itakombolewa.

Tumeangazia swala la unyanyasaji wa mwanamke na kuibuka pia na njia ambazo mwanamke anaweza kujikomboa kutokana na udhalimu wa viongozi na hasa jamii kwa jumla.Mwanamke anaweza kujikomboa kupitia njia zifuatazo: Kuelimika : Ni kupitia

kwa elimu ndipo mwanamke ataweza kugundua mambo mengi yakiwemo haki zake kama binadamu. Katango ni mwanamke ambaye ameelika. Anatambua matatizo yanayowapata wanawake waliokeketwa kama , shida za uzazi wakati wa kujifungua na hivyo kususia kukeketwa jambo ambalo halikumfurahisha babake. Mwanamke pia anaweza kusimama imara na kukashifu kaida alizowekewa na jamii na zinazodunisha utu wake.Mwanamke anafaa kuasi mila zilizopitwa na wakati kwa kuungana na kuhamasisha jamii kuasi tamaduni zilizopitwa na wakati na zisizofaa. Mwanamke anaweza kuwatambua na kuwashtaki wanajamii ambao wanaonekana kufaidi pekee yao kutokana na rasilmali ya jamii mwishowe jamii nzima itakombolewa.

### 4.1 Mapendekezo

Tumeliangazia swala la taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Kilio Cha Haki* (1981) kilichoandikwa na Alamin Mazrui na *Pango* (2003) kilichoandikwa na Wamitila K.W. Katika kushughulikia kazi hii tumetumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Tumeyaangazia matatizo yanayomkumba mwanamke katika jamii, jinsi mwanamke anavyojaribu kujikwamua kutoka kwa matatizo hayo na njia anazotumia kujikomboa.

Kipengele tulichokishughulikia kilihusisha taswira ya mwanamke, aidha tunaimani kuwa kuna vipengele ambavyo vinaweza kushughulikiwa kwa undani kuliko tulivyolishughulikia. Tunapendekeza pia tatizo la dhuluma ya mwanamke juu ya mwanamke mwenzake litafitiwe ili kubainisha pia mitazamo ya wanawake dhidi ya wanawake wenzao.

# MAREJELEO

Amadiume I. (1997) *Male daughters, Female Husbands: Gender and Sex in an African Society* Zed Books Ltd London.

Banks O. (1981). *Faces of Feminism. A study of Feminism as a social movement*, Basil Blackwell Ltd. London.

Barbara S. (1986). *Women in the Third World: A Historical Bibliography* Clio Press Ltd Oxford England.

Beauvoir S. (1953). *The Second Sex*, Penguin, Harmondsworth.

Broyelle C. (1977). *Women Liberation in China,*The Harvester Press Limited.

Bryden M. (1988). *Somalia Between Peace and War: Somalia Women on the Eve of the 21st Centuary*, Nairobi United Nations Development Fund For Women.

Brydon L and Chant S. (1993). *Women in The Third World.*:Edward Elgar Publishing Ltd. Gower House

Caroline F. (1963). *Feminine mystine* katika Gaskof M. *Roles Women Play.Brooks/Cole publishers Co: Belment(Calif)*

Dhahabu L. G. (1994). Uumbaji na Uendelezaji wa Wahusika katika tamthilia za Penina Muhando. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Engels F. (1985). *The Origin of the Family ,Private Property and the State*.Penguin Books Ltd Middlex

Freire P. (1972). *The Pedagogy of the Oppressed*. Penguin Books Ltd Middesex.

Friedman (1963). Katika Gaskof H: *Roles Women play*: *Reading towards women's liberation*. Brooks/Cole Publishers Co.:Belmont (Calif)

Garskof, M. (1971). *Roles Women Play: Reading Towards Women's Liberation*. Quinnipiac College.

Georgina .A. (1995). *A diplomacy of the Oppressed* Zed Ltd London.

Jaquette J. S. (1974). *Women in Politics* John Willey and Sons, New York.

Kamunde M.E. (1983). Kilio Cha Wanyonge Katika riwaya za Said Ahmed Mohammed.Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Katola E. (2006). Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Kathleen N. (1979). *The Sisterhood of Man :The impact of Womens' changing roles on Social and economic life around the world,* w.w. Norton, Publisher New York.

Kiango S. (1981). Maendeleo ya Uhusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili.Tasnifu ya M. A. Chuo kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Kisiroche R. K. (2008). Sauti ya Mwanamke Dhidi ya Ubabedume katika tamthilia tatu za Kiswahili.Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Kitsao J. (1980). *Uasi* Oxford University Press Nairobi.

Lugano R. (1989). "Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haikijachapiswa).

Mazrui A., 1981). *Kilio Cha Haki* Longman Publishers Nairobi.

Mbatiah, M. (2000). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphic and Publishing.

Mugambi P. J. (1982). Uhakiki wa maudhui katika tamthilia za Kenya zilizochapishwa.Tasnifu ya MA Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Ndung'o. M. (1985). Wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hakijachapishwa).

Njogu K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi:* Nadharia na Mbinu. Nairobi Jomo Kenyatta Foundation. Publishers.

Obbo C.(1980). *African Women :Their Struggle for Economic Independence*, Zed Press London.

Ogundupe . L. (1984). *African Women Culture and Another Development.* The Journal of African Marxists.

Ramazanoglu (1989). *Feminism and the Contradictions of Oppression.* London New York.

Retheun K. (1984). *Feminist Literary Studies.* Cambridge University Press, London.

Ruth, S. (1998). *Issues in Feminism – An Introduction to Women Studies.* Harmondworths: Penguin.

Sivard R.L (1985) Women a World Report Woshington DC:World Priorities.

Townsend J. (1988). *Women in Developing Countries: A selecting anointed Bibliography for Development Developed Bibliographies*. ID's Sussex .

TUKI (1981). *Kamusi ya KiswahiliSanifu* Dar es Salaam;Oxford University.

Wamitila (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus publishers.

________________ (2003). *Pango*. Focus Publishers .

________________ (2002). *Uhakiki wa Fasihi:* Msingi na Vipengele Vyake. Nairobi Phoenix.

________________ (2003). *Kamusi ya Fasihi:* Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publishers.